ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
51. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
52. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
54. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
56. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
61. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
66. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
67. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
68. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
69. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 2 Juni, 2017

(*Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha tarehe 29 Mei, 2017, Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na kuahidiwa kujibiwa kwa maandishi. Katika kutimiza masharti ya Kanuni ya 40(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, wizara hiyo imeleta majibu kwa Waziri wa Wizara hiyo kama alivyoahidi. Waheshimiwa Wajumbe, sasa namuomba Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo asome jibu la swali la nyongeza aliloulizwa na Mhe. Mjumbe huyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati ninajibu swali Nam.167 niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyetaka kufahamu ni kesi ngapi zilizofunguliwa Mahakamani na wahusika wa michezo kinyume na masharti ya wanachama wa *CAF*.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya kesi 4 zilifunguliwa Mahakamani na wahusika wa mchezo wa mpira wa miguu kinyume na masharti ya uanachama wa *CAF*, kesi zenyewe ni.

1. Kesi ya madai Nam. 62 iliyofunguliwa na aliyekuwa Makamu wa Rais *ZFA* Taifa Unguja Alhaj Haji Ameir Haji Mpakia dhidi ya viongozi wa *ZFA*.

2. Kesi ya madai iliyofunguliwa na Timu ya Aluta dhidi ya viongozi watatu wa *ZFA* Taifa akiwa ni Rais wa *ZFA*, Katibu Mkuu *ZFA* na Makamu wa Rais wa *ZFA* Pemba.

3. Kesi ya madai ya Timu ya Chuoni dhidi ya *ZFA* iliyopinga kuteremshwa daraja kwa timu hiyo.

4. Kesi ya madai dhidi ya *ZFA* kamati ya uchunguzi ya *ZFA* ndio iliyoshtakiwa kupinga kuongezewa muda kamati tendaji ya *ZFA* baada ya kupewa amri ya kusimamishwa (*stop order*) na Mahakama ya Mkoa wa Pemba. Kesi hii ilifunguliwa na Alhaj Haji Ameir Mpakia kwa mara ya pili kuzuia viongozi wa *ZFA* wasiongezewe muda na badala yake iundwe kamati ya muda.

Aidha, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alitaka kujua ni hatua gani zilizochukuliwa kuwaita waliofungua kesi hizo Mahakamani ili waweze kuziondoa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, hatua zifuatazo zilichukuliwa dhidi ya wahusika waliofungua kesi hizo Mahakamani zilizowasilishwa.

1. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, Baraza la Taifa la Michezo na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi walikutana na kuzungumza na ndugu Ali Haji Ameir na wadau wenzake na kutakiwa kuondosha kesi zote Mahakamani. Lakini kama hiyo haitoshi.

2. Muhusika mkuu ndugu Ali Haji Ameir alifukuzwa uongozi na mkutano mkuu wa dharura na kutakiwa kutogombea tena uongozi.

3. Uongozi wa Timu ya Chuoni na Aluta waliitwa na Baraza na *ZFA* na kufahamishwa wazi kuwa kwa mujibu wa masharti ya *CAF* kupeleka kesi za michezo Mahakamani ni kosa. Hivyo, walifahamu na waliondoa kesi zao zote mbili Mahakamani. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo hapa sote wenye afya njema na wazima. Naomba kuwasilisha hati mezani ya hotuba ya Wizara ya Afya kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2017/2018 katika Baraza lako tukufu la Wawakilishi. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa

Jamii, naomba kuweka hati mezani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2017/2018. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Afya

Mhe. Waziri wa Afya: *Bismilahi Rahman Rahiim.* Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako sasa likae kama Kamati ya Matumizi kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa tuna wajibu mkubwa wa kutanguliza shukurani zetu kwa Mola wetu Subhanahu Wataala, Muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima, tukaweza kukutana hapa leo sote tukiwa wenye afya njema na nchi yetu ikiwa na amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii adhimu kutoa pongezi maalum kwa Rais wetu mpendwa, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uongozi wake mahiri katika kuiongoza Zanzibar. Na namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, umri mrefu na ampe nguvu ya kuendelea kutuongoza kwa hekima na busara. Chini ya uongozi wake mahiri, serikali inaendelea kutekeleza kwa makini ahadi zake pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020 na katika Sekta ya Afya, Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein amefanikiwa kwa asilimia kubwa sana kutimiza ahadi zake zote alizotoa kupitia ilani hiyo na wakati alipotaka ridhaa ya wananchi wa Zanzibar. Hadi sasa, kwa upande wa ahadi zake katika mwaka wa kwanza amebakisha asilimia ndogo tu ya kutimiza ahadi alizotoa.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi zangu za dhati zimwendee Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa kuweza kusimamia vyema utekelezaji wa shughuli za serikali. Hotuba aliyoitoa kwenye Baraza lako wakati akiwasilisha hotuba yake ya bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18, ni kielelezo cha ukomavu wake katika uongozi na siasa. Hotuba hiyo imetoa muelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za serikali katika mwaka huu tunaokwenda nao wa fedha mpya.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mhe. Spika na Naibu Spika na Mwenyekiti mweza wako kwa kuliongoza vyema Baraza hili katika utekelezaji wa shughuli zake za kuishauri na kuisimamia serikali. Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa michango yao na miongozo yao mbali mbali ambayo imesaidia sana katika kuimarisha utendaji wa kazi zetu na kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Zanzibar. Ni matumaini yetu kuwa watazidi kutupa mashirikiano ili tuweze kupiga hatua zaidi katika kutoa huduma bora za afya kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Ustawi wa Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, Mwakilishi wa Jimbo la wananchi Dimani pamoja na Wajumbe wake, ambao ni Mhe. Tatu Mohamed Ussi, Makamu Mwenyekiti, Mwakilishi wa Viti Maalum, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani, Mhe. Viwe Khamis Abdalla ambaye amewasilisha hotuba ya kamati yake ambaye ni Mwakilishi wa Viti maalum, Mhe. Hidaya Ali Suleiman Mwakilishi wa Viti Maalum, Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud Mwakilishi wa Jimbo la Bububu ikiwemo na eneo la Mbuzini na Mhe. Makame Said Juma Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni.

Tunaishukuru kamati kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano mzuri na mwema wanaotupa katika utekelezaji wa kazi za wizara katika kipindi chote cha mwaka wa fedha 2016/2017, ikiwemo kupitia taarifa kuhusu muelekeo na malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Ushauri na maelekezo ya kamati hii na busara zao yametusaidia sana katika kuandaa hotuba hii ambayo leo mimi naiwasilisha hapa mbele yenu. Wizara ya Afya itaendelea kuzingatia ushauri wa kamati hii wakati tukitekeleza malengo yetu kwa mwaka ujao wa fedha. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati hii ambao ni Ndugu Khamis Hamad Haji na Ndugu Aziza Wazir Kheir pamoja na watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi waliokuwa wakitusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kutoa pongezi za pekee kwa wawakilishi wawili ambao wameteuliwa na Mhe. Rais baada ya kusoma bajeti yetu iliyopita nao ni Dkt. Sira Ubwa Mamboya na Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil. Naomba tumpongeze sana Mhe. Rais na niwapongeze hawa waheshimiwa kwa sababu uteuzi wake umeleta faraja kubwa kwa Wizara ya Afya. Dkt. Sira amekuwa akishirikiana na sisi kwa karibu sana tunampongeza pia kuchaguliwa Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum *member* wa Baraza La Mapinduzi , amekuwa akitusaidia sana na hasa katika fani yake ambayo wengi

hawaijui humu ndani, fani ya *Radiologia* ambayo inajumuisha moja kwa moja mashine zinazofanya uchunguzi katika hospitali zetu. Kwa hivyo, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana Dkt. Sira na Dkt. Ahmada Yahya Abdul-wakil.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii pia kuwapa pole wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, waliofikwa na maafa mbali mbali ikiwemo mafuriko yaliosababisha kuharibikiwa kwa makaazi yao pamoja na mali zao kutokana na mvua za Masika. Pia, nawapa pole wananchi wa Nyarugusu, Kinuni na maeneo mengine ambao nyumba zao ziliezuliwa mapaa na kuharibiwa kutokana na upepo mkali uliotokea siku ya tarehe 15 Mei, 2017. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subra katika kipindi hiki kigumu. Aidha, tunawapa pole ndugu na jamaa waliopoteza jamaa zao katika kipindi hiki cha mvua. Pia, tunatoa pole kwa Watanzania wote kutokana na ajali mbaya ya basi iliyotokea Mjini Karatu Mkoa wa Arusha tarehe 7 Mei, 2017 ambapo, ajali hiyo ilisababisha vifo vya watoto wa shule hiyo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho zao pahala pema peponi na awape afueni majeruhi wote wa ajali hiyo. *Amiin*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi, shukrani, na salamu za pole, naomba sasa uniruhusu nitoe maelezo ya mapato na matumizi, utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara ya Afya pamoja na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2016/2017.

MUHTASARI WA MAPATO APATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/17, wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 59. 22 ambapo kati ya hizo shilingi 17,332,500,000 ni kwa ajili ya mishahara na maposho; shilingi 1,496,600,000 kwa ajili ya ruzuku; shilingi 11,893,300,000 kwa matumizi mengineyo na jumla ya shilingi 28,506,231,000 ambapo shilingi 4,900,000,000 ni kutoka Mfuko wa Serikali na shillingi 23,606,231,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilitengwa kwa ajili ya kazi za maendeleo. Naomba mheshimiwa tu-*note* hapa kwamba katika mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao tulipata mchangio wa jumla wa shilingi bilioni 23 kutoka wafadhili wa maendeleo na hii inaonesha dhahiri kwamba wafadhili wa maendeleo wanaendelea bado kuiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyokuwepo madarakani bila ya wasi wasi wowote.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2017 wizara imeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 38,847,190,043 sawa na asilimia 65.6 ya fedha zilizotengwa. Kati ya hizo, shilingi 13,040,833,546 zimetumika kwa ajili ya mishahara na maposho, sawa na asilimia 75.2 ya fedha za mishahara zilizoidhinishwa, na shilingi 1,155,905,039 zimetumika kwa ajili ya ruzuku, sawa na asilimia 77.2 ya fedha zilizotengwa. Jumla ya shilingi 10,455,853,892 zimetumika kwa matumizi mengineyo, sawa na asilimia 87.9 ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya kazi hiyo. Kwa upande wa kazi za maendeleo, hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya shilingi 3,356,327,743 kutoka serikalini, sawa na asilimia 68.5 na shilingi 10,838,269,824 sawa na asilimia 45.9 ya fedha zilizoidhinishwa kutoka kwa washirika wa maendeleo zimetumika. Naomba tuangalie Kiambatisho Namba 1 kwa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizo zilitengwa kwa mujibu wa programu, ambapo maelezo yake yataelezwa katika kila programu husika. Pia, Wizara ya Afya ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 188,011,000 ambapo hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya shilingi 108,187,650 zimekusanywa sawa na asilimia 57.5. Kiambatisho Namba 2 kinatoa ufafanuzi wa vyanzo vya hivyo na makusanyo yake.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Hospitali ya Mnazi Mmoja iliidhinishiwa jumla ya shilingi 8,605,800,000 kwa kazi za kawaida, ambapo kati ya hizo, shilingi 7,470,800,000 ni kwa ajili ya mishahara na maposho na shilingi 1,135,000,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya shilingi 5,473,438,800 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya mishahara na maposho, sawa na asilimia 73 na shilingi 900,000,000 kwa matumizi mengineyo, sawa na asilimia 79 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, kwa upande wa mapato, Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipangiwa kukusanya shilingi 1,014,302,000, ambapo hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya shilingi 310,246,402 zimekusanywa sawa na asilimia 30.6.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017

Mhe. Mwenyekiti, wizara imetekeleza malengo yake kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo (2020) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA), Sera ya Afya (2011), Mpango Mkakati wa Wizara ya Afya 2013/14 – 2018/19, pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 - 2020. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya

Afya iliweka malengo yake kwa kutumia mfumo wa bajeti ya programu. Programu hizo ni kama zifuatazo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni programu nne tu ambazo tunazo katika Wizara ya Afya zinazosimamiwa na bajeti hii.

i. Programu ya Kinga na Elimu ya Afya;
ii. Programu ya Tiba;
iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya; na
iv. Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji kwa kila programu ulikuwa kama ifuatavyo:-

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA - H0101

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inahusisha utoaji wa huduma za kinga na elimu ya afya zinazotolewa katika vituo vya afya na vitengo mbali mbali. Programu hii, pamoja na shughuli nyengine, inajumuisha Mradi Shirikishi wa Afya ya Mama na Mtoto, Mradi Shirikishi wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma na Mradi wa Kumaliza Malaria hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/17, wizara ilitenga jumla ya shilingi 27,021,620,000 kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Programu ya Kinga na Elimu ya Afya, kati ya hizo shilingi 6,915,389,000 kutoka serikalini na shilingi 20,106,231,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya shilingi 4,895,545,570 sawa na asilimia 70.8 zilitumika kutoka serikalini na shilingi 4,238,269,823 sawa na asilimia 21.1 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Ufafanuzi zaidi wa programu hizo na michango yake unaonekana katika Kiambatisho Namba 3.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, programu ya Kinga na Elimu ya Afya ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuwajengea uwezo watendaji wa afya katika kutambua na kutibu magonjwa ya watoto;
ii. Kutoa huduma za chanjo kwa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano na wanawake walio katika umri wa kuzaa;

iii. Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya huduma za uzazi salama, chanjo, huduma za mama na mtoto na huduma za uzazi wa mpango;
iv. Kufuatilia vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga; na
v. Kudhibiti na kufuatilia maradhi ya miripuko, ya kuambukiza na yale ambayo yasiyo ya kuambukiza.

Mhe. Mwenyekiti, malengo haya yalitekelezwa kupitia miradi na huduma mbali mbali ni kama ifuatavyo:-

Huduma za Kinga Dhidi ya Maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma

Huduma hii inalenga kudhibiti ueneaji wa maradhi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma kwa kutoa huduma za kinga na tiba zinazohusiana na maradhi hayo. Jumla ya kliniki 12 (Unguja 8 na Pemba 4) zinatoa huduma za kinga na tiba kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI (VVU); kliniki hizo ni Mnazi Mmoja, Mwembeladu, Kidongo Chekundu, Makunduchi, Kivunge, Hospitali ya Jeshi Bububu, Al-Rahma na *ZAYEDESA* Miembeni kwa Unguja na Hospitali za Wete, Mkoani, Chake Chake na Micheweni kwa Pemba. Hadi kufikia mwisho wa Machi 2017, jumla ya wagonjwa 9,500 walikuwa wamesajiliwa kwenye kliniki hizo, miongoni mwao wagonjwa 7,213 (asilimia 76) walianzishiwa dawa za kupunguza makali ya VVU (*ARVs*), ambapo wagonjwa wanaoendelea kutumia dawa ni 4,576.

Mhe. Mwenyekiti, kazi nyengine iliyofanywa ni kukusanya sampuli za damu za watoto, ambao mama zao wameambukizwa na virusi vya UKIMWI kwa ajili ya uchunguzi. Jumla ya sampuli za damu za watoto 150 zimefanyiwa uchunguzi, kati ya hizo, 10 sawa na asilimia sita (6) zimegundulikana kuwa na maambukizo ya VVU kwa watoto hao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, watu 74,322 (wanaume 37,883 na wanawake 36,439) walichunguzwa katika vituo vya ushauri nasaha na upimaji wa virusi vya UKIMWI; kati yao 771 (asilimia 1.0) waligundulika kuwa na VVU. Watu hao wamechunguzwa katika vituo 110 vya Unguja na Pemba na kupitia huduma za masafa *(outreach services)*. Kwa jumla hadi hivi sasa Zanzibar naomba niseme ipo katika hali nzuri ya udhibiti wa maradhi ya UKIMWI, hali iliyopelekea kupongezwa kwa mbinu na njia za udhibiti tunazotumia hapa Zanzibar kwa Shirika la Afya ulimwenguni. Tunapongezwa sana kwa mbinu zetu tunazozitumia hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada za kupunguza athari kwa vijana walioathirika na dawa za kulevya, jumla ya vijana 324 wanaendelea kupatiwa dawa ya "*methadone*" katika kituo maalum kilichopo katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu. Kwa upande wa Kifua Kikuu, wagonjwa 557 **(**Unguja 360 na Pemba 197) waligundulika kuwa na maradhi hayo. Kati yao wagonjwa wanne (4) waligundulika na Kifua Kikuu sugu (*MDR TB*), ambapo watatu (3) walianzishiwa matibabu na mmoja anaendelea na kupatiwa ushauri nasaha.

Naomba maelezo yanayofuata yaendelee kuingia katika *hansard* yako Mhe. Mwenyekiti.

Takriban asilimia 89 ya wagonjwa waliogundulika na Kifua Kikuu mwaka 2015/2016 wamepona maradhi hayo. Sambamba na hilo, watu 948 katika maeneo waliyotoka wagonjwa 112 wa Kifua Kikuu walipatiwa elimu ya maradhi hayo, ambapo watu 383 walionekana kuwa na dalili za maradhi ya Kifua Kikuu na 13 waligunduliwa kuwa na Kifua Kikuu na kupatiwa matibabu. Katika zoezi hilo watoto 109 (Unguja 80 na Pemba 29) chini ya umri wa miaka mitano wamepatiwa dawa za kinga. Kulingana na matokeo ya utafiti wa kiwango cha Kifuu Kikuu (2012), ilikadiriwa kuibua wagonjwa wapya 1,612 kwa mwaka. Hadi kufikia Disemba 2016, wagonjwa 723 sawa na asilimia 45 ya waliokadiriwa waliibuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wagonjwa 56 (Unguja 53 na Pemba 3) waligundulika kuwa na ugonjwa wa Ukoma. Katika kupunguza ulemavu utokanao na Ukoma (*leprosy*), kati yao, wagonjwa 39 sawa na asilimia 69.6 walikuwa na ukoma mpevu (mabaka mengi) na 17 walikuwa na ukoma hafifu (mabaka machache). Naomba maelezo yanayofuata yaingie kwenye *hansard* mpaka hapo kifungu cha 24.

Zoezi la kuwafuatilia watu walioambukizwa na ugonjwa wa ukoma limefanyika katika Shehia mbili (2) za Kusini Unguja (Shehia ya Kizimkazi Mkunguni na Kizimkazi Dimbani) ambako ugonjwa huu umeenea kwa kiasi kwa lengo la kuwatambua wale ambao wanaweza kufanyiwa urekebishaji wa viungo. Katika zoezi hilo, watu 2,915 walichunguzwa, kati yao 106 waligunduliwa kuwa na maradhi ya ngozi na watu wawili (2) wamegunduliwa kuwa maradhi ya Ukoma. Matibabu stahiki walipatiwa wale wote waliogunduliwa na maradhi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya imeanzisha kitengo maalum chini ya Mradi Shirikishi wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma kinachoshughulika na Homa ya Ini (*Viral Hep B*). Kuanzishwa kwa kitengo hiki kumetokana na Shirika la Afya Ulimwenguni, kuzitaka Wizara za Afya zote Barani Afrika zisimamie suala hili kwa kuwa na vitengo vyake maalum kutokana na uzito wa tatizo lenyewe. Matokeo ya uchunguzi uliofanyika mwaka 2016 kwa makundi mbali mbali yanaonesha kuwa asilimia 1.7 ya wajawazito waliopimwa wameonekana kuwa na magonjwa hayo ya homa ya ini, wanaochangia damu asilimia mbili (2) na wanaojidunga dawa za kulevya ni asilimia 2.7. Maelekezo ya serikali pia yalipelekea kuanzishwa kwa kitengo hichi cha *Viral Hepatitis* (Homa ya Ini).

Huduma za Kumaliza Malaria Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, kazi za kinga na tiba dhidi ya ugonjwa wa malaria zinaendelea kwa kupata mafanikio chini ya kampeni ya “Maliza Malaria Zanzibar”, tunatoka kwenye ile Kampuni ya Kutokomeza sasa tunaingia katika kampeni ya "Maliza Malaria Zanzibar". Miongoni mwa mikakati inayotumika ni pamoja na usambazaji na ushajihishaji wa matumizi sahihi ya vyandarua, uchunguzi na tiba ya wagonjwa, elimu ya afya kwa jamii kuhusu kinga dhidi ya ugonjwa huu, ufuatiliaji wa wagonjwa katika ngazi ya Shehia na ufuatiliaji wa tabia na wingi wa mbu waenezao malaria hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kupungua kwa ugonjwa wa malaria kunatokana na ufuatiliaji wa huduma za uchunguzi na tiba sahihi ya malaria kwa wagonjwa, ambapo vituo vya afya 243 Unguja na Pemba vinatuma taarifa za malaria kwa kutumia simu ya mkononi. Jumla ya watu 394,766 waliochunguzwa malaria katika hospitali na vituo vya afya hapa Zanzibar, kati yao 5,874 sawa na asilimia 1.5 waligundulika kuwa na vimelea vya malaria; miongoni mwao asilimia 24.8 walikuwa watoto chini ya umri wa miaka mitano. Aidha, asilimia 80.8 sawa na watu 4,748 waliogundulika na vimelea vya malaria walifuatiliwa majumbani ili kuwachunguza jamaa wa wagonjwa hao kama na wao hawajaambukizwa na vimelea hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu zinatuonesha kuwa mwaka 2016/2017, Shehia tano (5) ndizo zilizoripoti wagonjwa wengi zaidi waliougua malaria; Shehia hizo ni Miwani, Fumba, Donge Karange, Donge Mbiji kwa Unguja na Tumbe Mashariki kwa upande wa Pemba. Vile vile Wilaya nne (4) zinaonesha bado maambukizo ya malaria yapo juu, nazo ni Wilaya ya Magharibi, Kati na Kaskazini B kwa Unguja na Micheweni kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, *trend* hii ya vimelea vya malaria katika maeneo haya yanaonesha pia kwamba watu wa eneo hili pia ni wanaosafiri sana. Naomba maelezo ya kifungu cha 28 yaingie kwenye *hansard*.

Uhakiki wa matokeo ya uchunguzi wa vimelea vya malaria umeendelea kufanyika, ambapo matokeo yameonesha kuwa asilimia 98.5 ya waliogundulika kuwa na malaria walithibitika kuwa na vimelea vya malaria na asilimia 99.9 hawakuwa na vimelea vya ugonjwa huo. Vile vile, mafunzo kwa maafisa ufuatiliaji pamoja na Timu za Afya za Wilaya juu ya kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji kwa wanaogundulika na malaria, yalifanyika kwa mashirikiano na Shirika la Afya Ulimwenguni.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuliarifu Baraza lako kuwa katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, hali ya upatikanaji wa dawa za malaria kwa wagonjwa ilikuwa nzuri na hakukuwa na upungufu wa dawa hizo kabisa hapa Zanzibar. Hii ni kutokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanza kununua dawa hizo sisi wenyewe badala ya kutegemea Washirika wa Maendeleo. Tayari tumeshaanza kujitegemea katika suala hilo. Hali hii, itatuwezesha kuongeza nguvu zetu katika udhibiti wa malaria hapa Zanzibar na kufikia malengo ya "Maliza Malaria Zanzibar". ZANZIBAR BILA MALARIA INAWEZEKANA! Na hii pia itakuwa ni kivutio kikubwa sana kwa utalii unaoingia hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kusisitiza mkakati wa kumaliza na kutokomeza malaria kabisa ni jukumu la kila mwananchi, katika ngazi zote kuanzia ngazi ya jamii, serikali, Washirika wa Maendeleo na mashirika binafsi. Hivyo, katika kufanikisha azma hiyo, wizara iliendelea na kudhibiti mbu waenezao ugonjwa wa malaria kwa kupiga dawa majumbani. Nyumba 38,884 kati ya 42,505 sawa na asilimia 91 zilipigwa dawa. Kabla sijaulizwa kwa nini nyengine hazijapigwa wengine walikataa kutoa mashirikiano yao lakini jitihada za kupiga dawa bado zinaendelea.

Zoezi hili lilifanyika katika maeneo maalum ya Wilaya za Magharibi, Wilaya ya Kati, Wilaya ya Kusini, Kaskazini A na Kaskazini B kwa Unguja na Chake Chake, Wete, Mkoani na Micheweni kwa upande wa Pemba. Aidha, uchunguzi wa uimara na uwezo wa dawa inayopigwa majumbani umeonesha dawa ya *"Actellic 300CS"* ina uwezo wa kubaki kwenye kuta za aina zote (za rangi ya mafuta, rangi ya maji, saruji, chokaa, kuta za *chipping* na udongo wa ufinyazi ambao huwa baadhi ya nyumba tunatumia). Kuta hizo zote zilizopigwa dawa zinakaa dawa hizo kwa muda wa miezi minane. Athari ndogo za kupata uwasho baada ya kupigwa dawa zilitokea pale wananchi wanapokosa kufuata

masharti wanayopewa na wataalamu wetu moja ikiwepo kuingia mapema kabla ya ule muda wa dawa ile kupoa ukutani kufikia.

Mhe. Mwenyekiti, vyandarua vyenye dawa ya muda mrefu viligawiwa kwa wananchi kwenye maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya vyandarua 702,185 (asilimia 89.3) kati ya vyandarua 786,757 viligawiwa kwa wananchi katika Shehia 334 kati ya Shehia 339. Utaratibu wa kugawa vyandarua hivi kwa Shehia tano (5) zilizosalia za Mkwajuni, Kivunge, Kilimani, Kilindi na Chaani Mcheza Shauri sasa hivi unaendelea. Mpango endelevu wa ugawaji vyandarua kwa mama wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja huu unaendelea hauhitaji muda maalum. Kwa hivyo, tunawashajihisha mama wajawazito na watoto kwena kufuata vyandarua hivyo. Mpaka kufikia mwishoni mwa Disemba 2016, jumla ya vyandarua vilivyogaiwa ni 98,669 kati ya vyandarua 185,205. Vyandarua vilivyosalia vinatarajiwa kufika nchini Zanzibar mwezi wa Agosti 2017. Mara tu vitakapofika vyandarua hivyo basi vitagawiwa kwa walengwa wote waliokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za ufuatiliaji wa tabia za mbu zilifanyika katika maeneo 10, maeneo hayo ni Donge Mchangani, Cheju, Bumbwini, Malindi, Muyuni na Mwera kwa Unguja na Bopwe, Tumbe, Uwandani na Wambaa kwa Pemba. Katika zoezi hilo mbu aina ya "*Anopheles arabiensi*" na "*Anopheles merus*" walikusanywa, uchunguzi wa vinasaba unaonesha mbu wa malaria wa aina ya *"Anopheles arabiensi"* kwa Unguja na Pemba yupo akifuatiwa na *Anopheles Meru* kwa visiwa vyetu. Aidha, tafiti zinaonesha kwamba aina zote za mbu hawa wana tabia ya kula na kupumzika nje bukheri wenyewe. Hivyo, wizara inatoa tahadhari kwa wananchi kutumia kinga wanapokuwa nje ya nyumba zao kwa muda mrefu hasa wale wenye vikao vya usiku zaidi. Kutokana na changamoto hii, njia za ziada za kumaliza malaria zinahitajika, zikiwemo kuangamiza viluilui katika maeneo yenye madimbwi na mabonde ya maji.

Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto

Mhe. Mwenyekiti, ni jukumu la wizara kuhakikisha kwamba mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano wanapata huduma bora za afya hapa Zanzibar, ili kufikia lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Jumla ya mama wajawazito 45,021 walipatiwa huduma za kupima ujauzito katika vituo na hospitali mbali mbali Unguja na Pemba, kati yao wajawazito 11,111 walifika katika muda unaoshauriwa na wataalamu wa afya katika vituo vyetu vya afya, ambao ni

ndani ya miezi minne ya ujauzito unatakiwa ufike. Muda huu unasisitizwa sana ili kuweza kugundua viashiria vyovyote vile vya hatari mapema na kwa wakati na kuweza kuchukua hatua stahiki. Wengine wote katika hao 45,021 ukitoa 11,111 hawakufika kwa wakati katika vituo vyetu vya afya.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wazazi 20,893 walijifungua katika hospitali na vituo vya afya. (Unguja 13,378 na Pemba 7,515). Kati yao wazazi 19,511 walijifungua kwa njia ya kawaida na 1,382 walijifungua kwa njia ya upasuaji kama **Kiambatisho Namba 4** kinavyoonesha.

Mhe. Mwenyekiti, vifo vya mama wajawazito bado ni tatizo katika jamii yetu, ambapo jumla ya vifo 27 vimeripotiwa katika Hospitali zetu za Unguja na Pemba, katika kipindi cha mwaka 2016/2017. Hata hivyo, idadi hiyo inaonekana kupungua ukilinganisha na kipindi kama hichi kwa mwaka 2015/16, ambapo jumla ya wajawazito 32 wakati huo waliripotiwa kufariki dunia. Sababu kuu zilizochangia vifo hivyo ni pamoja na kifafa cha mimba (*eclampsia*), ambacho kikigunduliwa mapema tunaweza kumuokoa mzazi, akichelewa ndipo kinapokuja juu zaidi. *Pressure* inayotokana na ujauzito (*pregnancy induced hypertension)*, pia nayo ukifika mapema kwenye kiliniki naweza kugunduliwa nayo, kupasuka kwa fuko la uzazi (*rupture of uterus)* nalo mara nyingi hutokea kutokana na kuchelewa kunakopelekea kupoteza damu nyingi na maambukizi wakati na baada ya kujifungua hutokea (*sepsis*). Hayo yote yanaweza kuepukika tukifika mapema na wakati mjamzito amefikwa na uchungu pia nayo kufika mapema asisubiri kwa dakika ya mwisho kufika kabla ya muda wake aliopangiwa katika vituo vya afya.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuiomba jamii yetu Zanzibar kuhudhuria vituoni kwetu vituo vya afya mara tu pale watakapoona kuna dalili zozote za viashiria vya hatari. Aidha, katika juhudi za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, wizara imefanya upanuzi wa vituo sita ili viweze kutoa huduma za uzazi na watoto wachanga**.** Vituo hivyo ni Tumbatu Gomani, Sebleni na Fuoni kwa hapa Unguja, Uondwe, Bogoa na Junguni kwa Pemba. Upanuzi huo umehusisha uwekaji wa vitendea kazi ambavyo ni pamoja na seti za kuzalishia, vitanda na jiko la kutakasa vifaa (*sterilizer*). Naomba maelezo ya kifungu cha 36 yaingie kwenye *hansard* Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali za Micheweni, Vitongoji na Wete pia zimefanyiwa ukarabati na kupatiwa vifaa vya huduma vya kuzalishia na huduma za watoto wachanga pamoja na ujenzi wa sehemu maalum za kuchomea taka za hospitali (*incinerators*). Vituo 13 vinavyotoa huduma za kuzalisha Unguja na 12 kwa Pemba vimeongezewa vifaa kwa ajili ya kuimarisha huduma za uzazi. Aidha,

Hospitali za Micheweni, Wete na Chake Chake kwa Pemba na Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu kwa upande wa Unguja zimepatiwa vifaa vya upasuaji na vya kuokolea maisha.

Mhe. Mwenyekiti, vituo kwa ajili ya kutoa huduma rafiki kwa vijana ikiwemo uzazi wa mpango, huduma za ushauri nasaha, kuchunguza virusi vya UKIMWI na elimu ya afya vimeanzishwa. Vituo hivyo ni Kituo cha Afya cha Mwera ambacho tayari kimeanza kutoa huduma hizo na vituo viwili vya Pemba Bwagamoyo na Mbuzini ujenzi wake unaendelea. Naomba maelezo ya kifungu cha 38 yaingie kwenye *hansard.*

Mhe. Mwenyekiti, watoa huduma za afya 40 wamefundishwa juu ya kutoa huduma mchanganyiko za uzazi wa mpango. Vile vile mafunzo ya utoaji wa huduma rafiki kwa vijana yametolewa kwa watoa huduma za afya 40 (Unguja 20 na Pemba 20). Aidha, wahudumu 251 **(**Unguja 163 na Pemba 88) walipatiwa mafunzo kuhusu huduma mchanganyiko za matibabu ya magonjwa ya watoto, wahudumu 158 **(**Unguja 98 na Pemba 60) wamepatiwa mafunzo ya huduma za watoto wachanga (njiti) na wahudumu 60 **(**Unguja 40 na Pemba 20) wamefundishwa juu ya huduma ya mama kwa njia ya kangaroo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Afya imeendelea kutoa chanjo kwa watoto walio chini ya miaka mitano na wanawake wenye umri wa kuzaa (miaka 15 hadi 49). Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya watoto 37,354 walipata chanjo tatu, naomba nirudie hili kwa manufaa ya baadhi ya Waheshimiwa pamoja na Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Hadi kufikia Machi 2017 jumla ya watoto 37,354 walipata chanjo tatu ya *Penta* 3, ya kujikinga na ugonjwa wa donda koo, kifaduro, pepopunda, *influenza "B"* na homa ya uti wa mgongo**.** Takwimu hizi zinaonesha wastani wa kiwango cha chanjo umefikia asilimia 78 kwa kwetu hapa Zanzibar, ambapo inaashiria uwezekano mkubwa wa kufikia lengo la kitaifa la asilimia 90. Kwa hiyo, lengo letu ni asilimia 90 tuko asilimia 78; tunajitahidi sana ili tuweze kufikia lengo hilo la asilimia 90. Pia, jumla ya wanawake 34,281 wamepata chanjo za kumkinga mama na mtoto ugonjwa wa pepopunda, kati yao 24,556 walikuwa ni mama wajawazito na 9,725 walikuwa wanawake walio katika umri wa kuzaa. **Kiambatisho Namba 5** kinatoa ufafanuzi zaidi juu ya huduma za chanjo.

Mhe. Mwenyekiti, ufanisi wa utoaji wa huduma yeyote ile unategemea pia kuwepo na miongozo imara itakayowasaidia watendaji katika utoaji wa huduma hizo kwa wananchi. Katika kipindi cha mwaka 2016/17, wizara ilitayarisha miongozo ifuatayo:-

i. Muongozo wa rufaa wa kusafirisha wagonjwa wanaohitaji huduma za dharura kutoka katika vituo vya afya ya msingi kwenda katika hospitali kuu yetu ya Mnazi Mmoja;

ii. Muongozo wa kushirikisha kina baba kushiriki katika huduma za afya za uzazi, hususan uzazi wa mpango; yaani tunalazimisha siku hizi baba aje kama haji wakati mwengine mama tutamrudisha lazima aje na baba. Kwa hivyo, na wanaume naomba mtoe mashirikiano yenu; na

iii. Muongozo wa kufundishia kufundishia wafanyakazi wa afya wanaotoa huduma rafiki kwa vijana.

Aidha matangazo wa ziada ya aina nne juu ya uzazi wa mpango na dalili za hatari kwa mama wajawazito yametayarishwa na kurushwa hewani kupitia redio na *television* zetu. Naomba maelezo ya kifungu cha 41 yaangie kwenye hansard Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua za kukinga maambukizi wa *VVU* kutoka kwa mama mjamzito kwenda kwa mtoto, jumla ya wajawazito 36,711....

Mhe. Mwenyekiti: Samanahi kidogo kabla ya kuendelea kuna tangazo, Wajumbe wa Kamati ya Bajeti baada tu ya kusikia tangazo hili wanatakiwa wafike katika ukumbi hapo juu baada ya tangazo. tuendelee.

Mhe. Waziri wa Afya: Niko kifungu cha 42 ukurasa wa 19 naomba nirudie.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua za kukinga maambukuzi ya *VVU* kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, jumla ya wajawazito 36,711 walichunguzwa afya zao katika klinik zetu mbali mbali za mama wajawazito na wodi za wazazi. Akina mama 92 tu ndio waliogundulika kuwa na *VVU* hivyo walipewa dawa za kupunguza makali yaani *ARV* ya *VVU* hivyo zisiende kwa mtoto. Aidha kati ya wenza wa mama wajawazito yaani waume zao ama wenza 2,165 waliopimwa *VVU*, hao tu ndio waliojitokeza wenzetu kule Tanzania Bara na mimi nilibahatika kuwatembelea katika klinik zao tayari baadhi ya kliniki wanarudisha akina mama wajawazito wasiokwenda na wenza wao. Kwa hiyo, kwenda na mwenza na muhimu sana hasa katika masuala ya *VVU* pakiweko na maambukizi. Aidha kati ya wenza wa mama wajawazito hao 2165 waliompimwa *VVU* 26 waligundulika kuwa na maambukizi ya virusi ya Ukimwi.

Huduma za kupambana na Maradhi yasiyoambukiza hapa Zanzibar *Non Communicable Diseases- NCDs*.

Mhe. Mwenyekiti, ambayo nayo sasa hivi yameendelea kuonesha kupanda na kushamiri kwa hapa kwetu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, udhibiti wa maradhi yasiyo ya kuambukiza ni suala mtambuka linalogusa nyanja mbali mbali, kwa kutambua hilo wizara imeanzisha kamati shirikishi inajumuisha Mamaktibu wakuu kutoka Wizara za Afya, Fedha, Kilimo, Elimu na Biashara pamoja na Mwakilishi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mwengine kutoka Shirika la Viwango Zanzibar. Haya yote ni katika kukinga na maradhi haya ndio maana huyu mtu wa viwango pia yupo kutokana na vyakula. Aidha Kamati Shirikishi ya kitaalamu itakayoratibu utekelezaji wa mikakati ya kupambana na maradhi haya itaundwa hivi karibuni na itakuwa inawasilisha taarifa za utekelezaji wake kwa Kamati Shirikishi ya Makatibu Wakuu hao. Ni matarajio yetu Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuanzishwa kwa kamati hizi kutasaidia kuratibu na kuhamasisha utekelezaji wa mikakati ya kupambana na maradhi haya ambayo hivi sasa hivi ni mengi na yanaendelea kupanda na wagonjwa wetu wengi tunawapeleka nje ya nchi ni wa maradhi yasioambukiza. Naomba maelezo ya kifungu cha 44 yaingie kwenye *hansard* yako.

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo juu ya uwezo wa kugundua na kutibu magonjwa ya kisukari, shindikizo la damu pamoja na magonjwa sugu ya njia ya hewa yametolewa kwa wafanyakazi wa afya 181 Unguja na Pemba. Aidha wafanyakazi 63 wanaohusika na klinik na maradhi ya kisukari walipatiwa mafunzo maalum ya kuhudumia wagonjwa wa kisukari hasa wale waliopata vidonda vinavyotokana na maradhi hayo ya kisukari.

Mhe. Mwenyekiti, njia moja inayotumiwa kuzidhibiti athari za maradhi haya ni kuwataka wananchi kupima afya zao mara kwa mara tunatakiwa sisi wananchi tuwe na tabia angalau kwa uchache kabisa mwaka mara moja kupima afya yako *full body checkup* na hii ifanyike mapema iwezekavyo. Katika kulitekeleza hili wizara pia iliendesha zoezi maalum la kupima afya za wafanyakazi wa serikali kwa wizara 13 tusiwe tunasema tu mfano mzuri uanzie kwetu sisi wenyewe. Jumla ya wafanyakazi 1,948 Unguja 977 na Pemba 971 wanawake wakiwa 1,026 na wanaume 922 walipimwa afya zao, kati yao asilimia 32 walionekana kuwa na viashiria vya kupata shindikizo la damu yaani asilimia 32 ya wafanyakazi hao wa serikali walionekana wako kwenye hatari maana shindikizo la damu linaweza kutokea wakati wowote ukapata matatizo wakati wowote ukaanguka wakati wowote, asilimia 6 walikuwa na ugonjwa wa

kisukari na asilimia 32 walikuwa na uzito uliozidi kiwango na asilimia 29 wao walikuwa na unene uliopindukia ama uliokithiri yaani *obesity*. Katika zoezi hilo wizara tatu 3 zilizoongoza kwa kuwa na kiwango cha juu cha sukari kwa wafanyakazi wao yaani wizara zisizokuwa na afya nzuri, wizara hizo ni Wizara ya Maji ya kwanza iliongoza ambayo ni Wizara ya Maji, Ardhi, Nishati na Madini wao kwa asilimia 11.5

Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilikuwa ya pili ambayo walionekana asilimia 7.6 wafanyakazi wote kuwa na viashiria hivi na Wizara ya Afya ilikuwa ya tatu kutokuwa na afya nzuri asilimia 7. Wizara nyengine zote wao walikuwa katika hali nzuri, kiambatanisho namba 6 mkienda kukiangalia mtakiona kinatoa matokeo ya uchunguzi huo kwa kila wizara.

Mhe. Mwenyekiti, maradhi haya yanaweza kuepukika iwapo wananchi watakuwa na tabia ya kufanya mazoezi na utaratibu mzuri wa mpangilio wa ulaji wa vyakula, ikiwemo vyakula vya mboga mboga na matunda, katika kushajihisha kufanya mazoezi wizara iliandaa mashindano ya mpira wa miguu na itaendelea kuandaa mashindano haya, wazira 8 zilishindanishwa katika mashindano haya. Timu ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo iliibuka kuwa ni bingwa mshindi na kukabidhiwa kikombe na zawadi naomba niwape pongezi Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. (*Makofi*)

Pia ulifanyika mdahalo ambao ulishirikishwa skuli 8 za Sekondari 6 zilikuwa za serikali na mbili za binafsi mada mbali mbali zinazohusiana na ungonjwa wa kisukari zilijadiliwa ngazi hizo za skuli ambapo Skuli ya Makunduchi, Mwanakwerekwe C na Vikokotoni ndio zilizotokea mabingwa na kwa upande wa Skuli binafsi ni Skuli ya Trifonia ilishinda na kutunukiwa vyeti na fedha taslimu.

Huduma za kupambana na Kichocho, Vikope, Minyoo na Matende

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwaambie Waheshimiwa Wawakilishi kwamba maradhi haya hivi sasa Umoja wa Mataifa unaita maradhi yaliokuwa hayajapewa kipaumbele kwa sababu yamebakia sehemu ndogo sana ya dunia na ndio maana yakaundiwa kundi maalum kundi la nchi tano na sisi Tanzania katika hizo nchi tano tukiwemo katika Kamati hiyo ya Umoja wa Mataifa tukiwa tunaingia katika Shirika la Afya Duniani katika maradhi haya. Maradhi haya yameonekana kwamba wanaweza kupigwa vita na yanaweza kuondoka kwa sababu kila moja huwa linasababu maalum ya kutokana na maradhi haya

na mengi ni kutokana na taabia sisi zetu wenyewe za kutofata yale masharti tunayopewa ama kutumia maji safi pale tunapotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, awamu ya kumi....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe**.** Waziri, samahani kidogo tulia Mheshimiwa hapo hapo. Waheshimiwa Wajumbe kuna taarifa kuhusu wageni ambao wametufikia hii leo wa kwanza naomba tumtambue Balozi wa Morocco karibu sana. (*Makofi*)

Lakini pia wageni wengine kutoka Wizara ya Afya wageni wa Mhe. Spika, wa Baraza la Wawakilishi ni huyo Balozi wa Morocco na Mgeni wenyewe ni balozi wa Morocco ni:

Balozi Abdelilah Benryawe. (*Makofi*)

Wengine ni wageni wa Wizara ya Afya nao naomba tuwatambue ni:-

1.	Mr. Xie Xioaw	-	Consul General of China
2.	Mr. Chen Li	-	Consul
3.	Dr. Andemichael G	-	WHO
4.	DR. Aduado Dalcourt	-	Cuban Medical Team
5.	Ms. Franchesca Morandini	-	UNICEF
6.	Mr. Jabir James	-	HIPZ
7.	Dr. Tosin Kuti	-	UNICEF
8.	Ms. Faiza Abbas	-	ZAMEP
9.	Ms. Batula Abdi	-	UNFPA
10.	Ms. Mali Nilsson	-	Save The Children
11.	Ms. Khadija Ahmed	-	Milele Foundation
12.	Dr. Xu Zhouqun	-	Chines Medical Team
13.	Ms. Zhu Yi	-	Chines Medical Team
14.	Ms. Lucy Ikamba	-	JHIEPIEGO

Karibuni sana wageni wetu, tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuwatambua hao naomba Baraza lako litambue kwamba kati ya zile bilioni ishirini na nne zitakazozisoma mwaka huu wachangiaji wetu wakubwa ndio kundi hili waliokuja hapa mbele yetu, hawa wanachangia jumla ya bilioni ishirini na nne kwa wananchi wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Machi 2017 jumla ya wagonjwa 517 waliogundulika na maradhi ya kichocho walipatiwa matibabu katika Vituo vya Afya vya Unguja na Pemba, shughuli za uzalishaji wa dawa za kichocho katika Skuli zilifanyika kisiwani Pemba ambapo jumla ya skuli 694 za Msingi, Sekondari na Madrassa zilifikiwa. Naomba maelezo yaliyobakia yote Mhe. Mwenyekiti yaangie katika *hansard* yako hadi kifungu cha 54 ambapo nitakwenda moja kwa moja kwenye unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa mtoto. Jambo linaloweza kuimarisha hali ya lishe ya mtoto.

Juhudi za kuhimiza unyonyeshaji watoto zinafanyika katika kliniki za mama wajawazito na watoto na katika siku maalum ya kuadhimisha siku ya kunyonyesha duniani. Hata hivyo bado muitikio wa kina mama kunyonyesha maziwa ya mama pekee ni mdogo kwani kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2015/2016 *Tanzania Demographic and Health Survey* ni asilimia 20 tu ya kina mama ndio wanaonyonyesha maziwa ya mama pekee kwa muda wa miezi 6 ya mwanzo kwa watoto wao.

Wizara inatoa wito kwa wazazi kuwanyonyesha watoto maziwa ya mama pekee kwa miezi 6 ya mwanzo tangu mtoto kuzaliwa na naomba Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla watuunge mkono katika kampeni hii ya kuhamasisha na kuwashajihisha wazazi kuwanyonyesha watoto maziwa ya mama pekee kwa miezi 6 ya mwanzo ili tufikie malengo ya asilimia 80 tuliyojiwekea. Mhe. Mwenyekiti, unyonyeshaji huu huongeza afya na kinga ya maradhi kwa mtoto moja kwa moja ndio faida moja kuu inayopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, ugawaji wa madini joto kwa uzalishaji wa chumvi uliendelea ambapo kilogramu 200 za madini hayo zilikabidhiwa kwa wazalishaji wa chumvi huko Pemba. Hata hivyo, matumizi ya chumvi yenye madini joto yako chini hasa kwa kisiwa cha Pemba asilimia 54 kwa Mkoa wa Kaskazini na asilimia 66 kwa Mkoa wa Kusini. Kwa upande wa Unguja matumizi ya chumvi yenye madini joto kwa Mkoa wa Kusini ni asilimia 85 Kaskazini ni asilimia 88 na Mkoa wa Mjini Magharibi asilimia 91 ambao ndio Mkoa wetu unaongoza kwa hapa Zanzibar kwa kutumia madini joto vizuri.

Wizara inatoa wito kwa wananchi kutumia chumvi yenye madini joto madini joto ndio nakusudia aidini ili kuwanusuru kupata maradhi ya tezi ya shingo, madini hayo ni hiyo aidini niliyoitaja na chumvi hiyo inakuwa na chapa iliyoandikwa *audios salt.*

Huduma za Afya Bandarini pamoja na Uwanja wa Ndege

Mhe. Mwenyekiti, ni kujumu la Wizara ya Afya kupitia maafisa afya walioko Bandarini kufanya ukaguzi kwa kila chombo kinachoingia kupitia bandari zetu, hadi kufikia Machi 2017 maafisa hao waliweza kufanya ukaguzi mara 1,253 katika Boti za kusafiria naomba maelezo yote yanayofuata yaangie kwenye *hansard* hadi kifungu 59 ambapo naingia kwenye huduma ya afya ya mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada ya kuikinga jamii na maradhi yanayoambukizwa kwa kupitia maji ya kunywa wizara imefanya uchunguzi wa sampuli 26 ya maji kutoka vyanzo mbali mbali vya maji hapa Zanzibar, matokeo yaliyoonesha kuwa sampuli 18 zilikuwa salama kwa matumizi ya binaadamu na sampuli 8 za vyanzo hivyo vya maji zilikuwa na vidudu vinavyosababisha maradhi, ambapo hatua za kutibu vianzo hivyo zilichukuliwa mara moja. Sambamba na hilo sampuli elfu 11,810 za maji kutoka kwa watumiaji mbali mbali majumbani wenye visima zilipimwa kuwa na uwepo wa dawa ya *chlorine* ambapo sampuli 9,845 zilionekana kuwa na *chlorine* ya kutosha na sampuli 1,965 hazikuwa na dawa hiyo za *chlorine* ya kutosha ambayo ni sawa na asilimia 17 na utaratibu wa kuyatibu maji hayo na vianzo hivyo ulifanyika mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya vidonge 79,200 vya dawa aina ya *Jumbo aqua tab* ya kutibu maji viligaiwa kwa wenye visima na matangi ya maji ambao hutoa huduma za maji kwa jamii inayowazunguka na wenye gari za kuuza maji. Naomba maelezo yanayofuata yote kwenye kifungu hicho yaaingie kwenye *hansard*.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wauza vyakula yaani *food vendors* 316 walikaguliwa. Kati yao 7 walinyanganywa vibali vyao kabisa na 62 walipewa onyo kali kutokana na masharti waliyopewa, ukaguzi huu ni endelevu na unafanywa kwa mashirikiano baina ya Maafisa wetu wa Wizara ya Afya na Maafisa wa Manispaa pamoja na Halmashauri mbali mbali kupitia Wizara yetu ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa.

Sambamba na hilo juhudi za kuwahimiza wananchi kujenga na kutumia vyoo bora pamoja na kunawa mikono inaendelea ambapo jumla ya vipindi 28 vya redio viliandaliwa na kurushwa hewani, jumla ya mikahawa 1,033 ilikaguliwa ambapo 700 ilionekana imetimiza masharti kuwepo kwa vyoo kwa ajili ya wateja wao na Mikahawa 337 haikuruhusiwa kabisa kufanya biashara kutokana na kutotimiza masharti hayo, pale watakaporekebisha mapungufu hayo

wanatakiwa kurudi na sisi tutaendelea kuwapa kibali cha kuendelea na biashara zao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema kwamba mafunzo ya mbinu Shirikishi Jamii kuhusu usafi ijulikanayo kitaaluma kama ni *Community Led Total Sanitation* yalitolewa kwa maafisa 40 kutoka *ZAWA*, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Kamati za Afya za Shehia ili kuishirikisha jamii katika suala zima la kujenga vyoo. Aidha wanafunzi 3,000 mashuleni walielimishwa juu ya umuhimu wa kutumia vyoo na kuosha mikono katika skuli mbali mbali za Unguja na Pemba pamoja na Programu inayoendelea kuoneshwa katika *TV* yetu za *ZBC* kwa ajili ya kinga hiyo ya kipindupindu.

Huduma za Ufatiliaji wa Mienendo ya Maradhi

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za ufatiliaji wa mienendo ya maradhi ya kuambukiza kwa kila wiki kutoka katika vituo vya afya ziliendelea kufanyika jumla ya wagonjwa 405 waliripotiwa kati ya 263 walikuwa wanaharisha damu, 137 walitafunwa na mbwa, wanne 4 waliugua surua na mmoja 1 alikuwa ugonjwa wa uvujaji damu mwilini yaani *VHF*. Naomba maelezo ya kifungu cha 64 na 65 yanayotoa ufafanuzi huo yaangie kwenye *hansard* yako.

Huduma za Ufuatiliaji wa Mienendo ya Maradhi

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya imeendelea kufuatilia mienendo ya maradhi kwa kutafuta sababu zilizopelekea kutokea kwa maradhi hayo pamoja na kuchukua hatua za kukabiliana nayo. Pia kukabiliana na majanga mengine ya kiafya yanayoikumba jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi yakiwemo maradhi ya Kuharisha, Surua, Kutafunwa na Wanyama, Homa ya Ini, Homa ya Matumbo, Tete Kuanga umefanyika kwa wilaya zote, **Kiambatisho namba 4 kinafafanua.**

Mhe. Mwenyekiti, ufuatiliaji huo wa maradhi umeenda sambamba na utoaji wa mafunzo kwa walimu **150** wa skuli za msingi na sekondari juu ya maradhi ya miripuko yanayoingia na yale yanayoibuka. Mafunzo hayo yanahusiana na kujenga uelewa juu ya maradhi hayo.

Huduma za Kupambana na Maradhi Yasiyoambukiza

Mhe. Mwenyekiti, maradhi yasiyoambukiza yanaonekana kuongezeka kwa kasi katika visiwa vyetu kwa miaka ya hivi karibuni. Magonjwa hayo ni pamoja na Shindikizo la Damu, Kisukari, Saratani, Ajali za barabani na magonjwa mengine sugu ikiwemo Pumu. Wizara ina jukumu.

Huduma za Elimu ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za afya katika skuli zetu zilitekelezwa kwa mafanikio makubwa sana katika mwaka wa fedha huu unaomalizika. Jumla ya skuli 143 Unguja 120 na Pemba 23 zenye wanafunzi 15,346 zimefanyiwa ukaguzi wa mazingira na kupatiwa elimu ya afya, mada zilizowasilishwa ni pamoja na maradhi ya kuharisha, kipundupindu, pepo punda, umuhimu wa unawaji mkono usafi wa mwili, usafi wa wasichana wakati wa hedhi na umuhimu wa chanjo kwa wanafunzi. Maneno haya inabidi yatamkwe katika Wizara ya Afya. Aidha, Muongozo Shirikishi wa Utoaji wa Huduma za Afya katika Skuli umetayarishwa ili kuimarisha utoaji wa huduma hizo. Naomba maelezo ya kifungu cha 67,68 na 69 Mhe. Mwenyekiti, yaingie kwenye *Hansard* yetu.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya afya kupitia vyombo vya habari ilifanyika, ambapo jumla ya matangazo 10 yalitangazwa mara 500 katika vyombo vya habari vya Serikali na binafsi. Aidha, vipindi 20 vya redio vyenye mada mbali mbali vilirushwa hewani, zikiwemo namna ya kujikinga na maradhi ya kipindupindu, lishe bora, utumiaji wa maji safi na salama, unyonyeshaji maziwa ya mama, umuhimu wa chanjo, uzazi salama, usafi wa mazingira na umuhimu wa unawaji mikono. Pia, vipeperushi 70,000 vinavyohusu umuhimu wa usafi na unawaji mikono vilisambazwa kwa wananchi Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, njia nyengine iliyotumiwa kufikisha elimu ya afya kwa jamii ni kupitia Kamati za Afya za Shehia, ambapo jumla ya Shehia 72 (Unguja 32 na Pemba 40) zimefikiwa na kuelimishwa juu ya maradhi ya mripuko, hasa kipindupindu. Ni mategemeo ya Wizara kuwa Kamati hizi zitafikisha elimu hiyo kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia vyombo vya habari, jumla ya vipindi 12 (asilimia 80) kati ya vipindi 15 vilivyopangwa vya redio na televisheni vilirushwa hewani kupitia *ZBC, Zenj FM*, Redio Mtegani na Micheweni. Elimu juu ya kumaliza malaria pia iliwahusisha Wakuu wa Wilaya, Madiwani,

Masheha, Mashekhe, Mapadri na Wasanii maarufu katika kampeni ya Maliza Malaria Zanzibar.

Huduma za Afya ya Macho ya Msingi

Mhe. Mwenyekiti, huduma za matibabu ya afya ya macho ziliendelea kutolewa katika hospitali na vituo vya afya. Pia, matibabu ya macho kwa watoto yalitolewa katika kambi maalum kwa mashirikiano makubwa na madaktari bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Jumla ya watoto 2,089 walichunguzwa zao za macho, kati yao 186 walifanyiwa upasuaji na 15 walipewa rufaa kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Tanzania Bara. Pia, kambi za matibabu ya macho zilifanyika katika hospitali ya Mnazi Mmoja na Wete, ambapo jumla ya wagonjwa 300 walifanyiwa upasuaji wa macho.

Mhe. Mwenyekiti, uchunguzi wa macho pia ulifanywa kupitia siku maalum za afya vijijini katika vituo mbali mbali, ambapo jumla ya watu 5,684 walichunguzwa afya zao za macho, (wanaume 3,261 na wanawake 2,423), ambapo watu 4,442 sawa na asilimia 78 walionekana kuwa na matatizo ya aina mbali mbali kama inavyoonekana katika Kiambatisho Namba 8.

Wizara imepokea vifaa vya matibabu ya macho kutoka kwa wenzetu wa "*Sight Savers International*" ambao nao walialikwa leo hapa, na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, *Lion Club na Spectacle Saver*. Vifaa hivyo ni mashine za uchunguzi wa presha ya macho, mashine za uchunguzi wa miwani pamoja na mashine za kufanyia upasuaji wa matibabu ya macho. Vifaa vyote hivyo viligharimu jumla ya Shilingi 78,765,898.

Huduma za Afya ya Akili ya Msingi

Mhe. Mwenyekiti, huduma masafa (*out reach services*) za afya ya akili ziliendelea kutolewa katika hospitali zote za Vijiji na Wilaya kwa Unguja na Pemba. Jumla ya ziara 33 zilifanyika, ambapo wagonjwa 697 (wanaume 320 na wanawake 377) wenye matatizo ya afya ya akili walipatiwa huduma karibu na maeneo wanayoishi.

Sasa naomba niingie kwenye programu ya pili kuu, programu ya tiba.

PROGRAMU YA HUDUMA ZA TIBA (H0102)

Mhe. Mwenyekiti, programu ya huduma za tiba imegawika katika programu ndogo mbili kuu;

a) programu ndogo ya huduma za uchunguzi inayohusisha shughuli za:-

i. Huduma za udhibiti wa Kemikali, Chakula, Dawa na Vipodozi; na
ii. Huduma za uchunguzi wa Maabara na Mionzi.

b) programu ndogo ya huduma za matibabu ambayo inajumuisha:

i. Huduma za Upatikanaji, utunzaji na usambazaji wa dawa; na
ii. Huduma za Mpango wa Damu salama.

Aidha, programu hii pia, inahusika na Mabaraza na Bodi mbali mbali ambazo ni:-Mabaraza ya Wauguzi na Wakunga, Ofisi ya Muuguzi Mkuu Kiongozi, Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi na Bodi ya Madaktari. Pia, programu hii inatekeleza Mradi wa Kupandisha hadhi Hospitali za Vijiji kuwa za Wilaya na Wilaya kuwa za Mkoa. Lengo la program hii ni kuimarisha utoaji wa huduma bora zenye viwango na ufanisi katika hospitali zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ilitenga jumla ya Shilingi 11,230,180,000 kutoka Serikalini kwa ajili ya uendeshaji wa programu ya Tiba. Hadi kufikia Machi 2017, Shilingi 10,968,107,134 sawa na asilimia 97.7 zilitumika katika programu hii ya tiba.

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo ya kifungu cha 75,76,77,78 na 79 yaingie kwenye *Hansard* yako.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za utoaji wa matibabu ni moja ya jukumu la msingi la Sekta ya Afya. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara katika Programu ya Huduma za Tiba ilijiwekea malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha upatikanaji wa dawa muhimu, zana na vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali na vituo vya afya;
ii. Kumalizia kuandaa rasimu ya Sheria ya Bohari Kuu ya Dawa;
iii. Kuendelea na mchakato wa ujenzi wa Bohari ya Dawa Pemba;
iv. Kuendelea kuimarisha mifumo ya uendeshaji wa kazi za Bohari katika kuhifadhi na kusambaza dawa;
v. Kumalizia ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee; na
vi. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi.

Mhe. Mwenyekiti, malengo yaliyoainishwa katika program hii yalitekelezwa kupitia programu ndogo mbili kama ifuatavyo:-

Programu ndogo ya Uchunguzi

Huduma za Udhibiti wa Kemikali, Dawa, Vifaa tiba, Chakula na Vipodozi

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Bodi ya Chakula, Dawa na vipodozi ilikagua jumla ya maeneo 1,088 sawa na asilimia 86.1 kati ya maeneo 1,264 ya biashara za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba iliyojipangia. Jumla ya tani 86.3 ziliteketezwa na Bodi hiyo, zikiwemo tani 82.3 za bidhaa za chakula na tani 4 za dawa na vipodozi zisizofaa kwa matumizi ya binadamu, ambazo zilikamatwa wakati wa ukaguzi. Uchambuzi wa aina ya bidhaa na jumla ya tani zilizoteketezwa unavyoonekana katika Kiambatisho Namba 9.

Aidha, jumla ya tani 125 za sukari zisizofikia kiwango cha ubora kwa matumizi zilirejeshwa katika nchi zilikotoka. Pia, bodi imeweza kukagua viwanda 16 vilivyopo katika nchi za Urusi, Ukraine, Afrika Kusini, India, Kenya, China na Oman ambavyo bidhaa zake zinaingizwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa usajili, jumla ya maeneo 739 ya biashara/uzalishaji wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba yamefanyiwa tathmini na kusajiliwa. Aidha, jumla ya bidhaa 16 zikiwemo chakula, dawa na vifaa tiba zimesajiliwa. Jumla ya sampuli 958 zikiwemo 911 za chakula, 24 za vipodozi na 23 za dawa za mitishamba zilichunguzwa katika maabara. Katika uchunguzi huo hakukuwa na sampuli yeyote iliyoonekana haifai kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi pia iliweza kushiriki kikamilifu katika Mpango Uwiyano wa Usajili wa Dawa kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kufanya ukaguzi wa pamoja (*Joint Good Manufacturing Practice Inspection*) kwenye viwanda vya dawa, ambapo jumla ya viwanda vinne (4) vimekaguliwa. Pia, tathmini ya pamoja (*Joint Dossier Evaluation*) ya bidhaa za dawa 16 imefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha ufanisi na utendaji wa shughuli za udhibiti wa ubora na usalama wa chakula, dawa na vipodozi, Wizara imefanya marekebisho katika Sheria Namba 2 ya mwaka 2006, ili kuifanya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi iwe Wakala wa Serikali. Mswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo tayari umeshapitishwa na Baraza hili mwezi wa Februari, 2017 na maelezo yake yalitolewa ya kina. Kwa hivyo, sina haja ya kusoma kifungu cha 81 na 81, naomba yaingie kwenye *Hansard*.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara ilifanya uchunguzi wa vielelezo 496, ambapo vielelezo 421 kutoka Jeshi la Polisi na 75 kutoka kwa watu binafsi. Miongoni mwa vielelezo vinavyochunguzwa hutumika katika kutoa ushahidi wa kesi mbali mbali zinazoendeshwa Mahakamani. Kiambatisho Namba 10 kinatoa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli nyengine zilizofanyika ni ukaguzi na usajili wa kemikali zinazotumika majumbani na viwandani, maghala ya kuhifadhia kemikali, sehemu za kuchanganyia kemikali pamoja na waingizaji, wasafirishaji na wauzaji wa kemikali, ambapo vyeti vya usajili vilitolewa kwa waliofikia viwango vilivyowekwa. Kazi ya ukaguzi wa mizigo ya kemikali kwa wasafiri wa bandarini pia ilifanyika. Aidha, vibali 514 vya kuingiza kemikali nchini vimetolewa.

Mhe. Mwenyekiti, kazi za ujenzi wa jengo la ghorofa moja la Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali iliyoanza mwezi wa April 2016, limefikia katika hatua za kukamilika hivi sasa. Kazi zinazoendelea kwa hivi sasa ni utiaji wa rangi, kuweka sakafu ya vigae na kuweka njia za umeme. Nashukuru Kamati ya Ustawi wa Jamii ilitembelea pia jengo hilo. Jengo la Maabara hiyo linategemewa kukamilika na kukabidhiwa kwa wizara mwishoni mwa mwezi wa Juni 2017. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tutafanya ufunguzi rasmi pale na *Inshaallah* tutawaalika Baraza la Wawakilishi zima.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa maabara ya Mkemia Mkuu Pemba, Wizara imeamua kulifanyia matengenezo jengo lililokuwa likitumika kwa kazi za Mradi wa Malaria liliopo Madungu, ili litumike kwa shughuli za maabara. Kazi hiyo ya matengenezo imekamilika na tayari jengo hilo linatumika kwa shughuli za maabara na ofisi za Mkemia Mkuu kisiwani Pemba.

Huduma za Uchunguzi wa Maabara na Mionzi

Mhe. Mwenyekiti, huduma hizi zinajumuisha huduma za uchunguzi wa Maabara pamoja na Radiolojia zinazotolewa katika hospitali mbali mbali za Unguja na Pemba. Katika mwaka wa fedha 2016/17, rasimu ya awali ya Sheria na Sera ya Huduma za Maabara imetayarishwa. Aidha, ufuatiliaji wa uwepo wa vifaa tiba vya uchunguzi pamoja na vitendanishi katika maabara mbali mbali ulifanyika. Jumla ya vipimo 145,006 vya uchunguzi wa magonjwa mbali mbali

vilifanyika katika hospitali za Serikali, ambapo vipimo vya maabara vilikuwa 103,708 na mionzi ni 41,298.

Program ndogo ya Huduma za Matibabu

Huduma ya Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ya Afya iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 4,903,400,000 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vifaa vya uchunguzi wa mionzi kutoka mfuko wa Serikali. Hadi kufikia Machi 2017, Wizara imepatiwa Shilingi 2,636,466,667 sawa na asilimia 53.8 ya fedha zilizotengwa. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo, dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi bilioni 4,635,884,378 hizi ni miongoni mwa zile 24 nilizozitaja, zilipokelewa. Dawa na vifaa hivyo ni kwa ajili ya huduma za UKIMWI, Malaria, Lishe, Uzazi wa Mpango na huduma za uzazi kama ilivyofafanuliwa katika Kiambatisho Namba 11.

Mhe. Mwenyekiti, naomba vifungu 87,88 na 89 viingie kwenye *Hansard*.

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo yenye lengo la kuimarisha upatikanaji sahihi wa hesabu za dawa yamefanyika kwa Wafamasia kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalihusisha mfumo mpya wa ujazaji wa fomu za maombi ya dawa katika vituo kwa njia ya kielektroniki, ambayo itasaidia upelekaji wa maombi sahihi ya dawa na vifaa pamoja na udhibiti wa matumizi ya dawa. Aidha, kompyuta 10 zilipokelewa kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kuimarisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika uendeshaji wa kazi za Bohari Kuu ya Dawa,

Mhe. Mwenyekiti, rasimu ya Sheria ya kuifanya Bohari ya Dawa kuwa ni Taasisi yenye kujitegemea imetayarishwa na iko katika hatua za kuwasilishwa katika ngazi mbali mbali. Kukamilika kwa Sheria hii kutaiwezesha Bohari Kuu ya Dawa kufanya kazi za upatikanaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa Bohari ya Dawa kisiwani Pemba, mradi ambao ulitarajiwa kugharamiwa na Serikali ya Watu wa Marekani kupitia Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*) haukufanyika kutokana na mabadiliko ya utawala katika nchi hiyo. Hata hivyo, Serikali inaendelea na jitihada za utafutaji wa fedha za ujenzi huo, na mara tu zikipatikana ujenzi utaanza mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikichukuwa jitihada mbali mbali za kudhibiti matumizi pamoja na upotevu wa dawa na vifaa kwenye hospitali na vituo vya afya Unguja na Pemba. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Ofisi ya Mfamasia Mkuu imefanya ukaguzi wa kina katika hospitali mbili (2) na vituo vya afya 131, sawa na asilimia 83 ya vituo vilivyopangwa kukaguliwa. Matokeo yameonesha kwamba dawa na vifaa zinatumiwa kwa mujibu wa miongozo tuliyoipanga. Hata hivyo, kuna mapungufu yaliyoonekana, yakiwemo ujazaji wa taarifa zisizo sahihi kwenye fomu za maombi, jambo linalopelekea hospitali au kituo cha afya kuishiwa na dawa mapema, ama kabla ya wakati wake au kuchelewa kupata dawa nyengine kutokana na makosa ya kujaza fomu hizo na dawa hizo kuchelewa kufika katika vituo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, hatua mbali mbali zimeshaanza kuchukuliwa zikiwemo kuanzisha huduma ya upatikanaji wa dawa kwa masaa 24 kwenye wodi ya wazazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Tangu huduma hii ianzishwe, upatikanaji wa dawa na vifaa katika wodi ya wazazi ya Hospitali ya Mnazi Mmoja umeimarika. Nia ya Wizara ni kuanzisha huduma za dawa katika hospitali zote Unguja na Pemba kadri hali ya upatikanaji wa wafanyakazi hasa hawa wafamansia itakavyoridhisha. Aidha, Serikali imeajiri mafundi sanifu wa dawa 34, ambao tayari wameshapangiwa kazi sehemu mbali mbali kwa lengo la kuimarisha huduma za dawa.

Mhe. Mwenyekiti, Huduma za Tiba zinaendelea kutolewa kwa Hospitali ya Chake-Chake, ambapo shughuli zilizofanyika ni pamoja na kufanyika kwa kambi za matibabu. Jumla ya kambi 11 ziliendeshwa na madaktari kutoka Mashirika na Jumuiya mbali mbali za ndani na nje ya nchi, ambapo wagonjwa 1,396 walihudumiwa (wanaume 872 na wanawake 524). Pia, hospitali imepokea vifaa mbali mbali vikiwemo vifaa vya upasuaji na uchunguzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa hospitali ya Wete, matengenezo makubwa yamefanyika katika chumba cha kusafishia filamu za "*x-ray*" na sehemu mapokezi na kliniki ya pua, koo na masikio. Aidha, shughuli nyingine zilizofanyika ni utoaji huduma za afya kwa maradhi mbali mbali katika kambi maalum.

Katika kambi hizo wagonjwa 547 wamefanyiwa upasuaji wa pua, koo na masikio na 37 wamepatiwa matibabu

Naomba maelezo yanayofuata yote Mhe. Mwenyekiti, ya kifungu cha 94,95 na 96 yaingie kwenye *Hansard* yetu pamoja na maelezo ya kina na ufafanuzi yaliyokuwa katika kiambatanisho nambari 12.

Mhe. Mwenyekiti, miundo mbinu ya maji safi imejengwa upya katika Hospitali ya Vitongoji. Ujenzi huo umesaidia kupatikana kwa maji ya uhakika, na hivyo tatizo la maji lililokuwepo kwa muda mrefu limepatiwa ufumbuzi. Aidha, matengenezo madogo madogo ya maeneo mbali mbali ya hospitali hiyo yamefanyika. Pia, ujenzi wa Kituo cha Mkono kwa Mkono umefanyika katika Hospitali ya Micheweni ili kutoa huduma kwa waathirika wa udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha miundombinu ya Hospitali ya Makunduchi, majengo mawili na wodi nne zimefanyiwa ukarabati pamoja na ujenzi wa Kituo cha Mkono kwa Mkono. Aidha, jengo la Hospitali ya Kivunge limefanyiwa ukarabati katika maeneo mbali mbali yakiwemo sehemu ya kutolea dawa, kituo cha Mkono kwa Mkono, sehemu ya mionzi na maabara, pamoja na kuwekwa tarazo katika hospitali yote.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya wagonjwa wa nje 418,468 (wanaume 222,118 na wanawake 196,350) na wagonjwa waliolazwa 22,651 (wanaume 5,582 na wanawake 17,069) waliripotiwa katika Hospitali za Abdalla Mzee, Chake Chake, Wete, Vitongoji na Micheweni kwa Pemba na Kivunge na Makunduchi kwa Unguja, ambapo wagonjwa 355 wamefariki dunia. Aidha, jumla ya wagonjwa 269,021 waliripotiwa kuhudumiwa katika kliniki za magonjwa maalum. Takwimu za wagonjwa waliohudumiwa katika hospitali hizo zinaonekana katika Kiambatisho Namba 12.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wazazi 8,937 walijifungua katika hospitali hizo, ambapo wazazi 8,368 walijifungua kwa njia ya kawaida na 569 walijifungua kwa njia ya upasuaji. Kati ya wajawazito 10,161 waliopokelewa katika hospitali hizo, 17 wamefariki dunia.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeendelea kuwafanyia uchunguzi wagonjwa wanaostahiki kupelekwa nje ya Zanzibar kwa matibabu. Hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya wagonjwa 114 walisafirishwa nchi mbali mbali kwa ajili ya matibabu. Wagonjwa 92 walipelekwa India kwa gharama na fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, 20 Tanzania Bara, mmoja (1) Afrika Kusini na mmoja (1) China. Jumla ya Shilingi 4,139,202,677 zilitumika kwa kugharamia

safari na matibabu ya wagonjwa hao nje ya Zanzibar kwa kutumia fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Huduma za Mpango wa Damu Salama

Mhe. Mwenyekiti, uhamasishaji wa wananchi juu ya kuchangia damu kwa hiari umeendelea, ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ilijipangia kukusanya uniti za damu 10,500 kutoka kwa wachangiaji wa hiari. Hadi kufikia Machi 2017, uniti 7,000 sawa na asilimia 66 zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa magonjwa ya UKIMWI, kaswende na homa ya Ini kabla ya kupelekwa katika hospitali mbali mbali kwa matumizi na baada hapo zilitumika.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kueleza hapo awali kwamba programu hii pia inahusisha shughuli za Bodi na Mabaraza yaliyomo ndani ya Wizara, hivyo, naomba uniruhusu nitowe maelezo ya utekelezaji wa huduma za taasisi hizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama ifuatavyo:-

Kabla sijatoa maelezo haya naomba niwashukuru waheshimiwa wote pamoja na wananchi wote, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa kushajihisha wananchi katika uchangiaji wa damu salama. Nawashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, uongozi wa Baraza pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi.

Huduma za Usimamizi wa Hospitali Binafsi

Mhe. Mwenyekiti, kazi kuu ya Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi ni kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa hospitali na vituo vya afya binafsi. Aidha, bodi hii ina jukumu la kuzikagua na kuzipatia maelekezo hospitali binafsi juu utoaji wa huduma za afya kwa mujibu wa taratibu na Sheria zilizopo. Bodi pia, imepewa uwezo wa kusimamisha ama kufunga hospitali binafsi, pale vigezo na miongozo inayotakiwa inapokiukwa. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2017, jumla ya hospitali na vituo vya afya binafsi 70 Unguja na Pemba vimepatiwa usajili na kutambuliwa rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya hospitali na vituo vya afya 50 vimekaguliwa, ambapo hospitali 10 zilipewa onyo kali kwa utoaji huduma kinyume na Sheria na miongozo ya uendeshaji wa hospitali hizo. Aidha, hospitali 12 zilisimamishwa ama kufungiwa kutoa huduma, kufuatia wamiliki kwenda kinyume na miongozo yetu tuliyoweka sheria za kuendesha hospitali hizo binafsi. Baadhi ya hospitali hizo ziliruhusiwa kuendelea na utoaji wa huduma,

baada ya wahusika kutekeleza maagizo ya bodi ya kuondoa kasoro zilizoonekana.

Huduma za Uratibu wa Wauguzi na Wakunga

Mhe. Mwenyekiti, shughuli za kusajili na kuratibu wauguzi na wakunga ziliendelea kwa kusajili jumla ya wauguzi na wakunga 983, ambapo hapo awali walikuwa hawana usajili, ikiwa pamoja na kuwapatia leseni zao, maana hawa wanapatiwa leseni kama vile dereva wa gari na yeye anapewa leseni kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa, hawezi kufanyakazi bila ya leseni.

Baraza la Wauguzi na Wakunga limetembelea hospitali sita (6) za Serikali; zikiwemo Hospitali ya Abdalla Mzee, Wete, Chake Chake, Vitongoji na Micheweni kwa Pemba na Mnazi Mmoja kwa Unguja. Pia, imetembelea hospitali tano (5) za binafsi zilioko Pemba ili kusimamia na kufuatilia utendaji wa wauguzi hao kwa mujibu miongozo na kanuni ziliopo. Hospitali hizo ni Selem, Baja, Dira, SDA na Mwanamashungi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme na nitamke wazi kwa Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, bodi hii ndio yenye uwezo wa kisheria ya kusimamia nidhamu na maadili ya wauguzi wote wanaotoa huduma katika Wizara ya Afya, pamoja na kufuta leseni zao. Humu mna mtu wa Mwanasheria Mkuu katika bodi hii anaingia moja kwa moja kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, wao ndio wenye mamlaka ya kuzuwia, kuwasimamisha na kuwanyang'anya leseni. Kwa hivyo, malalamiko yote hayo yanatakiwa yaende kwenye bodi hii na iko pale pale upande wa *Global Hospital opposite* kwenye ofisi yao, ambapo malalamiko yanatakiwa yawasilishwe pale.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya malalamiko matatu (3) ya utendaji kazi wa wauguzi yaliwasilishwa katika Baraza la Wauguzi na Wakunga. Malalamiko hayo yalifanyiwa uchunguzi na kutolewa maamuzi ya kisheria stahiki kwa wahusika, ambapo barua za onyo la maandishi zilitolewa kwa baadhi ya wahusika, na baadhi ya wahusika walisimamishwa kazi kwa muda.

Aidha, wauguzi watatu (3) wamefutiwa usajili wao na leseni zao kutokana na sababu za kughushi vyeti vya kumalizia mafunzo yao ya Uuguzi. Juzi tulisikia Bara huko wauguzi 199 walikamatwa na wengine walifutiwa. Katika kuongeza uelewa juu ya maadili ya wauguzi, nakala 90 za vitabu vya maadili viligawiwa kwa wauguzi, wakunga na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Tunatoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuifikisha ujumbe huu

na taaluma hii kwa wananchi, ili wawe na uelewa na kutoa taarifa pale inapobainika kutokea kwa uvunjifu wa maadili.

Naomba kuwaaambia Waheshimiwa Wawakilishi, hasa wale wanaotembea maeneo ya hospitali zaidi, wanapoona matatizo wao ni sehemu ya viongozi wa nchi hii, mwakilishi ni kiongozi. Pale pale wewe ukiwa ni mwakilishi basi unatakiwa kumwambia muuguzi unavyofanya sivyo, tutapeleka taarifa hizi. Sio kusubiri kuja kuleta taarifa baadae, kwa sababu na wewe ni kiongozi na sheria hii na maadili haya yametolewa na vitabu vyote hivi vimetolewa kwa Waheshimiwa Wawakilishi. Kwa hivyo, tunatarajia katika hili ni jukumu letu sote tutasaidiana pamoja. *(Makofi)*

Pili, naomba taarifa zozote zinazokuwepo za malalamiko zifikishwe moja kwa moja katika bodi, kwa sababu kisheria wao ndio wahusika. Malalamiko hivi sasa yanawasilishwa wizarani, aidha kwa Waziri au Naibu Waziri ama Katibu Mkuu, ama Naibu Katibu Mkuu ama Mkurugenzi Mkuu. Kisheria malalamiko yote yanayohusiana na wauguzi ama huduma za hospitali ama maadili ama uvunjifu ama kitoto kichanga kuachwa, ama mengine yoyote yanatakiwa yawasilishwe kwenye bodi hiyo ambapo Mwenyekiti wake ni Dk. Amina Abdul-kadir *Professor*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ndani ya bodi hiyo wako wajumbe mbali mbali wanaoteuliwa. Bi Amina anateuliwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein, wajumbe anawateua Waziri wa Afya. Ndani ya bodi hiyo kuna wajumbe wanaingia kwa nafasi zao, wanatokea katika vyombo mbali mbali vya ulinzi na usalama wa serikali. Pia wamo wanaoingia kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, naomba nikukumbushe kwa mujibu wa kanuni zetu, una dakika zilizobaki kama 10.

Mhe. Waziri wa Afya: Pamoja na zile ulizochukuwa wewe Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ni saa moja na nusu kwa mujibu wa kanuni zetu 96, unatakiwa uhutubie hotuba yako kwa saa moja na nusu. Kwa hivyo, sasa naona nikutahadharishe kuwa umebakisha kama dakika 10.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Naomba yaliyobakia yote hayo mpaka kifungu cha 110 yaingie kwenye *Hansard*. Maelezo hayo tayari nimeshayatolea na mengine nitayatolea nitakapopata nafasi ya kuulizwa kwa

ufafanuzi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ambapo ni wajibu wao pia kutaka ufafanuzi kwa niaba ya wananchi.

Nakwenda moja kwa moja kwenye Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja PH02.

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha 2016/2017, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala limeweza kuongeza idadi ya waganga waliosajiliwa kwa mujibu wa taratibu, vigezo na masharti kama ifuatavyo: Vilinge 196, Waganga 334, Wasaidizi Waganga 52, Kliniki 36 na Maduka ya dawa za asili 75. Aidha, Baraza limetayarisha muongozo kwa watabibu wa tiba za asili juu ya kufanya vipindi katika vyombo vya habari. Muongozo huo utasaidia katika kuweka utaratibu mzuri juu ya kutoa elimu ya afya za tiba za asili kwa jamii.

Huduma za Usajili wa Madaktari

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia julai 2016 hadi Machi 2017, Baraza la Madaktari limeweza kusajili jumla ya madaktari 64. Madaktari hao wamejumuisha madaktari wa kawaida (*Medical Doctors*) 56 na madaktari bingwa wa magonjwa mbali mbali wanane (8) wakiwemo; madaktari wa moyo, magonjwa ya akili, upasuaji wa mifupa, maradhi ya watoto na maradhi ya njia ya mkojo. Mapitio ya Sheria ya Madaktari Namba 12 ya mwaka 1999 pia yamefanyika.

Mradi wa Kupandisha Hadhi Hospital Wilaya na Vijiji

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 nilieleza kwamba ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee utakamilika na kukabidhiwa rasmi kwa Serikali mnamo mwezi wa Septemba 2016. Napenda kuliarifu Baraza lako kwamba Hospitali hiyo iliyojengwa upya na kuwekewa vifaa vipya na vya kisasa imekamilika na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, tarehe 26 Novemba 2016. Kukamilika kwa hospitali hii ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; Ukurasa 175 Ibara ya 102 (C) ya kuwapelekea huduma bora za afya wananchi wake karibu na maeneo yao wanayoishi.

Mhe. Mwenyekiti, jengo la hospitali hiyo ambalo ujenzi wake umegharimu jumla ya dola milioni 16, linajumuisha sehemu za ofisi, huduma za dharura (*casuality*), wagonjwa wa nje *(out-patient*), uchunguzi wa maabara, *x-ray, CT*

scan, EEG na Ultra sound, stoo ya kuhifadhia dawa, wodi ya wagonjwa mahtuti, vyumba vinne vya upasuaji, wodi nyinginezo mbali mbali, chumba cha kuhifadhia maiti pamoja na sehemu ya kuchomea taka. Aidha, napenda kuchukuwa fursa hii kuliarifu Baraza lako kuwa hospitali hiyo kwa sasa imepandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, natoa shukrani za dhati kabisa kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, kwa msaada wake katika ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee. Serikali ya Watu wa China wamekuwa wakishirikiana nasi kwa muda mrefu, na kwa kweli uhusiano uliopo baina ya Zanzibar na China ni wa kindugu na kihistoria. Pia, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza kwa mara nyengine Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye kikao chake na Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Dr. Xi Jinping ndicho kilichozaa na kuibua msaada huu mkubwa wa Hospitali mpya ya Abdalla Mzee. Ujenzi huu wa Hospitali ya Abdalla Mzee, umepelekea Mheshimiwa Rais, kutimiza ahadi yake nyengine kwa wananchi wa Zanzibar kwa wakati uliopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Abdalla Mzee, Wizara tayari imeshafanya mazungumzo ya awali na Wizara ya Fedha ili kuona njia za kupata fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Wizara ya Fedha tayari imeiandikia rasmi Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuomba msaada kwa ajili ya mradi huo. Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetenga Shilingi 1,000,000,000 kwa ajili ya kugharamia baadhi ya gharama za ujenzi wa nyumba hizo.

PROGRAMU YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (H02)

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja nayo inaendesha shughuli zake kwa mpango wa utekelezaji wa programu, ambapo inasimamia programu ndogo mbili; ambazo ni:-

a) Programu Ndogo ya Huduma za Uchunguzi na Matibabu; na
b) Programu Ndogo ya Uongozi wa Hospitali na Utawala.

Kwa kuwa Mnazi Mmoja itazungumziwa sana na itachangiwa sana nina uhakika na hilo, naomba vifungu 112,113,114,115,116,117 na 118 vyote viingie katika *Hansard* na ninaamini wajumbe watavisoma kwa kina na uchangiaji wao utakuwa mzuri sana kwa Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kifungu cha 119,120,121,122,123,124,125,126,127 na128 naomba viingie kwenye *Hansard*. Lakini kifungu cha 128 nitaomba

kidogo nikisome, kwa sababu hiki ni kifungu maalum na kinatoa huduma mpya maalum kwa Zanzibar, ambayo ni huduma ya *dialysis* kusafisha mafigo kwa kutumia mashine ambazo namshukuru Mhe. Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein amekuwa na mchango mkubwa sana wa kutupatia mashine hizo mpya zilizofika katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja. *(Makofi)*

Aidha, utekelezaji wa programu hii unahusisha Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hospitali ya Wazazi ya Mwembeladu na Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongo Chekundu, pamoja na Mradi wa Kuipandisha Hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja ndio tegemeo kubwa la wananchi wa Zanzibar katika kupata huduma zilizo bora, hususan zile za rufaa au zilizoshindikana katika hospitali nyengine hapa Zanzibar. Wizara katika kuimarisha huduma zitolewazo katika hospitali hii, ilipanga malengo yafuatayo katika mwaka 2016/2017:

i. Kuimarisha huduma za uchunguzi ikiwemo kuweka mashine ya "MRI", "*X-ray"* na *"ultrasound*";
ii. Kuimarisha huduma za tiba kwa kuanzisha huduma mpya ya kusafisha damu kwa wenye matatizo ya figo, ikiwemo ununuzi wa Mashine za "Dialysis";
iii. Kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba;
iv. Kuweka mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu za wagonjwa (*Electronic Medical system*);
v. Kuziimarisha kambi za matibabu kwa kushirikiana na madaktari kutoka nje ya nchi, ili kupunguza gharama kubwa zinazotumika kusafirisha wagonjwa nje ya nchi;
vi. Kukarabati jengo lililokuwa kiwanda cha dawa liliopo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya utoaji wa huduma za mama na mtoto yenye uwezo wa vitanda 112;
vii. Kuendelea na ujenzi wa wodi mpya ya watoto itakayokuwa na vitanda 100; na
viii. Ukarabati wa jengo la macho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ilitenga jumla ya Shilingi 1,135,000,000 kwa ajili uendeshaji wa shughuli za programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya Shilingi 900,000,000 sawa na asilimia 79 zilitumika.

Programu Ndogo ya Uendeshaji na Utawala ya Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Spika, Baraza lako lilipitisha Sheria Namba 3 ya mwaka 2016 ya kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe inajitegemea. Kufuatia kupitishwa kwa Sheria hiyo, mabadiliko makubwa ya kimuundo na kiutawala yamefanyika, ambapo hivi sasa hospitali inaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, ikisimamiwa na Bodi ya Ushauri. Bodi hiyo yenye wajumbe wanane (8) imeundwa baada ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kumteuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo Dk. Abdul-wakil Idrisa Abdul-wakil. Hatua inayofuata ni kuundwa kwa Idara nane (8) za hospitali, ambazo zinatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeendeleza mashirikiano na taasisi mbali mbali za kimataifa, ikiwemo mashirikiano mapya na Hospitali ya "Drum Tower ya China", ambayo itasaidia kutoa ujuzi wa kitaalamu wa huduma za mama na mtoto kwa muda wa miaka mitatu. Jumla ya wauguzi watano (5) na madaktari watano (5) wamepatiwa taaluma ya vitendo nchini China, na kila baada ya miezi mitatu wataalamu kutoka China wanakuja kuwapatia mafunzo kazini na kufuatilia maendeleo yao. Aidha, mashirikiano na Hospitali ya Chuo Kikuu cha "Haukeland" yanaendelea na kundi la saba (7) la wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja wanaendelea kupatiwa mafunzo ya vitendo nchini Norway.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukidhi mahitaji ya wataalamu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, Wizara ya Afya imewapeleka madaktari wa fani tofauti kwa ajili ya masomo ya digrii ya pili, kupitia mpango wa masomo wa muda mrefu. Jumla ya wafanyakazi 21 wamepelekwa masomoni kwa ajili ya fani mbali mbali za kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafunzo ya muda mrefu, wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja pia wamepatiwa mafunzo mbali mbali ya muda mfupi, kwa lengo la kuongeza ujuzi na ufanisi wa kazi za utoaji huduma za afya kwa jamii; mafunzo hayo yanajumuisha:-

i. Mafunzo kwa wafanyakazi wawili (2) juu ya huduma ya "Dialysis" katika Hospitali ya Muhimbili;
ii. Mafunzo ya awali ya wiki mbili ya "*Radiographers*" kwa wafanyakazi wanne (4) juu ya utumiaji mashine ya "*MRI" na "digital X-ray*";
iii. Mafunzo ya kujikinga na maambukizi, utoaji mzuri wa huduma za mama na mtoto, uongozi na utawala kwa ngazi mbali mbali; na

iv. Mafunzo ya "*Emergency Care*" kwa wafanyakazi mbali mbali, mafunzo hayo yaliyotolewa na madaktari kutoka Uingereza.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na huduma za matibabu, hospitali hii pia inatoa mafunzo ya vitendo (*Internship*) kwa wahitimu wa masomo ya udaktari kutoka katika vyuo na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi. Jumla ya madaktari 23 waliomaliza masomo yao walipokelewa na kupatiwa mafunzo ya vitendo. Aidha, wanafunzi kutoka Vyuo vya Taaluma za Afya tofauti wamepokelewa kwa ajili ya mafunzo ya vitendo, wakiwemo kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*Zanzibar State University – SUZA*), Chuo Kikuu cha Zanzibar *(Zanzibar University) na "Zanzibar School of Health".*

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, hospitali imekuwa ni kituo muhimu cha kufanyia tafiti za kuimarisha huduma za afya kutoka vyuo vikuu vya ndani na nje ya Tanzania. Jumla ya tafiti mbili zinaendelea kufanyika kuhusiana na maradhi ya Kifua Kikuu na uchunguzi wa homa ambazo sio malaria.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeweza kupata wataalamu wapya, ambapo madaktari bingwa watatu (3) wazalendo wamerejea kutoka masomoni. Madaktari hao ni; daktari bingwa wa upasuaji wa mishipa ya fahamu, ubongo na uti wa mgongo; daktari bingwa wa matibabu ya saratani; na daktari bingwa wa matibabu ya watoto. Kuwepo kwa madaktari hao bingwa, kunaifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja kuweza kuimarisha huduma zake katika maeneo hayo.

Pia, hospitali imepokea wauguzi wataalamu watatu (3) wa afya ya akili na muuguzi mmoja mtaalamu wa huduma za kina mama ambao wote hao tayari wameshaanza kazi. Aidha, wauguzi 31 wa shahada ya kwanza wamerudi masomoni na kuanza kazi. Haya yote yamepelekea kuongezeka kwa idadi ya wataalamu tuliokuwa nao kwa huduma za rufaa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kumalizika kwa jengo la wodi ya watoto ni hatua muhimu, ambayo inatowa nafasi nzuri kwa wagonjwa na kupunguza msongomano wa watoto kulala wawili wawili katika kitanda kimoja. Pia, kuweko na mazingira mazuri ya kazi kwa watendaji wetu. Hivi sasa wodi ya watoto ina vitanda 100 na ikibidi kuongeza tutafanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja imepatiwa jenereta tatu (3) zitazotumika pindi umeme utakapozimwa. Pia, jenereta jengine jipya lenye uwezo mkubwa (KVA 400) limepatikana kwa msaada wa *UNFPA*. Mtambo wa kuzalishia "*oxygen*" umefungwa na umeshaanza kutumika. Aidha, mashine ya

utakasaji wa vifaa vya upasuaji imewekwa katika chumba cha upasuaji ili iweze kusaidia kupunguza hatari ya maambukizi kwa wagonjwa na wafanyakazi.

Programu Ndogo ya Uchunguzi na Matibabu

Mhe. Mwenyekiti, huduma za uchunguzi ni sehemu muhimu ya kumsaidia daktari kuweza kuelewa maradhi yanayomsumbua mgonjwa na hatimae kumpatia matibabu sahihi na kwa wakati muafaka. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya vipimo vya uchunguzi 54,930 vilifanyika, vipimo hivyo vinajumuisha uchunguzi wa *X-ray* (12,529), CT-Scan (2,770), Ultra sound (11,850) na vipimo vya maabara (27,781)

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha huduma za uchunguzi, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeweza kupata na kuweka vifaa vipya, vikiwemo:-

i. "*Mobile X-ray*" mbili (2) na "*digital X-ray"* moja (1) ambazo tayari zimeshaanza kufanya kazi;
ii. Mashine mbili (2) za "Ultra sound" ambazo zimeongezwa kutokana na mahitaji ya huduma hii na ongezeko la wagonjwa;
iii. Mashine ya kisasa ya uchunguzi wa maradhi ya "*MRI*" ambayo ina uwezo mkubwa wa kuchunguza maradhi yaliyojificha ndani ya mwili wa binadamu; na
iv. Mashine ya maabara ya kuchunguzia damu.

Mhe. Mwenyekiti, hadi Machi 2017, jumla ya wagonjwa wa nje 114,208 (wanaume 48,641 na wanawake 65,567) na wagonjwa waliolazwa 20,921 (wanaume 4,887 na wanawake 16,034) waliripotiwa katika hospitali za Mnazi Mmoja, Mwembeladu na Kidongo Chekundu. Kiambatisho Namba 13 kinachanganua taarifa hizo kwa kila hospitali. Aidha, wazazi 9,733 walijifungua katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu, kati yao, wazazi 8,920 walijifungua kwa njia ya kawaida na 813 walijifungua kwa njia ya upasuaji.

Mhe. Mwenyekiti, huduma za matibabu katika kliniki maalum za Hospitali ya Mnazi Mmoja zikiwemo meno, macho, masikio, koo na pua, maradhi ya mifupa, maradhi ya kinamama, maradhi ya kisukari, shinikizo la damu, saratani na kliniki za ubongo na uti wa mgongo ziliendelea kutolewa. Takwimu za mahudhurio ya wagonjwa zinaonyesha kwamba jumla ya wagonjwa 49,868 walipatiwa huduma katika kliniki hizo, kati yao wanaume 21,062 na wanawake 28,806.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma za matibabu hapa hapa Zanzibar, na kuipunguzia Serikali gharama za kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi, Hospitali ya Mnazi Mmoja imeendesha kambi za matibabu kwa kushirikiana na madaktari bingwa kutoka nje ya nchi. Kambi ya watoto wenye matatizo ya moyo iliendeshwa na jumla ya watoto 265 walichunguzwa na 26 walifanyiwa upasuaji. Aidha, jumla ya watoto 13 walipelekwa India na 18 Israel kupatiwa matibabu ya moyo. Jitihada hizi za Serikali, zimesaidia sana kuokoa maisha ya watoto hawa ambao wazazi wao hawana uwezo wa kumudu gharama za matibabu nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, mashine za kusafishia damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo tayari zimeshafungwa, Hospitali ya Mnazi Mmoja na hivi sasa leo hii asubuhi *test* ya mwanzo kwa mgonjwa wa kwanza imeshaanza tayari, naomba kwa wale wanaopenda kutembelea pale maeneo yale watembelee na haya wapate kuyaona, Wataalam wetu wameazimia kupata mafunzo hayo na tayari wameshapata mafunzo hayo kutoka Dar es Salaam, na muda si mrefu hivi sasa tutaanza kazi rasmi, mgonjwa huyu wa leo wa kwanza amejitolea yeye kwa sababu mashine ni mpya na yeye mwenyewe amejitolea amesaini pale kwamba zile *test* zetu za mwanzo zote tufanye na yeye.

Huduma hizi sote tunajua huko Tanzania Bara zinatolewa kwa bei gani si chini ya laki tatu na nusu na watu walikuwa wakihangaika wanakwenda wiki mara moja, wiki mara mbili, wiki mara tatu, Tanzania bara sasa huduma hizi tunashukuru Mwenyezi Mungu katujaalia na tunamshukuru Rais wetu kwa kutusogezea huduma hizi kupatikana hapa Zanzibar na kuwa karibu na wananchi wa Zanzibar. Wataalamu wetu wanamalizia mafunzo ya utumiaji wa mashine hizo, na muda si mrefu wataanza kazi. Kupatikana kwa huduma hii kutasaidia wagonjwa wetu kuweza kupata tiba za awali za matatizo ya figo hapa Zanzibar.

Mradi wa Kupandisha hadhi Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Mwenyekiti, nilieleza katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya ya mwaka 2016/17, kwamba Serikali ina nia ya kukarabati jengo la kiwanda cha dawa cha zamani kilichopo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya utoaji wa huduma za uzazi. Nachukua fursa hii, kuliarifu Baraza lako kwamba ukarabati wa jengo hilo umekamilika na limeshaanza kutoa huduma hizo. Pia, ujenzi wa wodi za watoto katika hospitali hiyo umekamilika. Majengo hayo yenye vifaa vipya, vikiwemo vitanda na mashine mbali mbali yalizinduliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, tarehe 11 Novemba, 2016. Hii pia, ni miongoni mwa

ahadi za Mheshimiwa Rais alizotoa kupitia Ilani ya CCM na kuweza kutimizwa kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ukarabati wa jengo la macho, mchakato wa zabuni pamoja na mkataba wa ujenzi tayari umekamilika. Kazi ya ujenzi itaanza muda wowote kuanzia sasa. Tunaomba wananchi na wafanyakazi wawe wavumilivu wakati ujenzi huu unaendelea. Aidha, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa uongozi na wananchi wa Jimbo la Shauri Moyo kupitia Mwakilishi wao Mheshimiwa Hamza Hassan Juma kwa mashirikiano wanayotupa kufanikisha utoaji wa huduma za matibabu ya macho hapa Zanzibar.

PROGRAMU YA USIMAMIZI WA SERA ZA AFYA NA UTAWALA (H0103)

Mhe. Mwenyekiti, programu ya Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala yaani H0103 ambayo nayo itachangiwa kifungu 131, 132, 133,134 hadi 143 naomba viingie vyote hivi katika *Hansard.*

Mhe. Mwenyekiti, programu ya usimamizi wa sera za afya na utawala inalenga kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyopo na kwa kuzingatia misingi ya uwazi, uwajibikaji, ushiriki na ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa maamuzi kwenye ngazi zote. Programu hii inajumuisha Programu Ndogo tatu, nazo ni:-

a) Uongozi na Utawala;
b) Sera, Mipango na Utafiti; na
c) Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa usimamizi bora, upatikanaji wa rasilimali watu na uwajibikaji katika kazi ndio msingi mkubwa wa kufanikisha dhamira na nia ya Serikali katika kutoa huduma bora za afya. Katika kuimarisha usimamizi wa sera na utawala, Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17, ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kukamilisha matayarisho ya Mfuko wa Bima ya Afya na uanzishwaji wake;
ii. Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Tatu wa Afya 2013/14 – 2018/19;
iii. Kuratibu ukarabati wa vituo 19 vya afya ya msingi; na
iv. Kuimarisha nguvu kazi ya Sekta ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Wizara ilitenga jumla ya Shilingi 20,976,831,000 kwa ajili utekelezaji wa shughuli za Programu ya Usimamizi wa Sera za Afya na Utawala, kati ya hizo Shillingi 12,976,831,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 8,000,000,000 kwa kazi za maendeleo Shilingi 4,500,000,000 ni kutoka Serikalini na Shilingi 3,500,000,000 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2017, ni Shilingi 18,745,267,515 sawa na asilimia 89.4 zilitumika**.** Kati ya hizo, Shilingi 8,982,711,078 (asilimia 69.2 ni kwa matumizi ya kawaida ya fedha zilizopangwa kutoka Serikali. Aidha, Shilingi 9,762,556,437 (asilimia 122) zilitumika kwa kazi za maendeleo, kati ya hizo Shilingi 3,162,556,437 kutoka Serikali na Shilingi 6,600,000,000 kutoka kwa washirika wa Maendeleo.

Programu ndogo ya Uongozi na Utawala

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2016/2017**,** wafanyakazi 143 wa kada mbali mbali walipelekwa masomoni ndani na nje ya nchi katika fani mbali mbali yakiwemo masomo ya wataalamu bingwa *Nephrology, Anaesthesiology, Dermatology, Emergence Medicine, Obstetrics & Gynaecology, Othopedic Surgery, Pathology, Nuclear Medicine na Radiology*. Pia, wafanyakazi 150 wamerudi kutoka masomoni na kupangiwa kazi kwa mujibu wa taaluma zao.

Mhe. Mwenyekiti, nathubutu kusema kwamba, hapajapatapo kutokea, katika historia ya Wizara ya Afya kusomesha idadi kubwa ya madaktari bingwa 50 kwa wakati mmoja kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Namba 14 kinaonyesha. Hii pia, ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuwasomesha wafanyakazi mbali mbali ili kuongeza taaluma na idadi ya wataalamu ndani ya Sekta ya Afya. Mkazo na msisitizo uliowekwa na Mheshimiwa Rais, Dk. Ali Mohamed Shein, kufikia idadi ya kuwa na madaktari, kwa uwiano wa daktari mmoja kwa wagonjwa 6,000 (1:6,000) ni lengo la Afro Shirazi Party *(ASP)* na baadae kurithiwa na *CCM*.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeajiri wafanyakazi 101, kati yao madaktari 40, Mfamasia mmoja (1), wauguzi 13, Fundi Sanifu Dawa 43, Afisa Tabibu watatu (3) na Afisa wa Afya ya Mazingira mmoja (1). Aidha, wafanyakazi 107 wamestaafu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma (Unguja 48 na Pemba 59). Vile vile wafanyakazi 15 (Unguja **7** na Pemba **8**) wamefariki dunia; Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema, Amin.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wanafunzi 515 (wanaume 189 na wanawake 326) wa kada mbalimbali wamehitimu masomo ya Stashahada ya Uuguzi na Ukunga, Afisa Tabibu, Sayansi za Afya ya Mazingira, Famasia, Afya ya Kinywa na Meno na Maabara katika Chuo cha Sayansi za Afya Mbweni, kama Kiambatisho Namba 15 inavyoonesha. Pia, jumla ya wanafunzi wapya 454 wamesajiliwa katika muhula wa masomo wa 2016/2017. Sambamba na hayo, Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya Mbweni, kimeunganishwa rasmi na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar *(SUZA)*, chini ya Sheria Namba 7 ya mwaka 2016 iliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi, ambapo makabidhiano yalifanyika rasmi tarehe 16 Januari, 2017.

Programu Ndogo ya Sera, Mipango na Utafiti

Mhe. Mwenyekiti, nilieleza katika hotuba ya Wizara ya Afya ya mwaka 2016/2017 kwamba Wizara inatayarisha Sheria kwa ajili ya kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar. Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Baraza hili kwamba rasimu ya awali ya mswada wa Sheria imekamilika. Rasimu hii imejadiliwa katika vikao mbali mbali na watendaji katika sekta ya umma na sekta binafsi. Hatua inayofuata ni kuwasilisha mapendekezo ya rasimu hiyo katika Kamati ya Makatibu Wakuu na baadae Baraza la Mapinduzi, kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi. Uanzishwaji wa Bima ya Afya Zanzibar, ni kutekeleza maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; ukurasa wa 176, Ibara ya 102 (l). Serikali tayari imetenga Shilingi 2,000,000,000 ikiwa ni fedha za kuanzisha mfuko *(Seed money)*, ambapo bima hiyo itaanza kwa watumishi wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba mipango inayopangwa na Wizara inatokana na ushahidi wa kitakwimu, mafunzo kwa watendaji wa Timu za Afya za Wilaya juu ya jinsi ya kupanga mipango yao kwa kutumia ushahidi wa kitakwimu unaotokana na uchambuzi wa vikwazo viliopo yaani *Bottleneck Analysis* yalifanyika**.** Sambamba na hilo, Mkataba wa Makubaliano ya Mfuko wa Fedha za pamoja wa Afya Wilayani *District Health Basket Fund* na Akaunti ya Mfuko wa Dawa Muhimu *Essential Medicine Account* imeunganishwa kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya wilayani.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu ya program ndogo ya Sera, Mipango, na Utafiti ni kutoa miongozo juu ya kupanga mipango ya Wizara kwa kila mwaka. Katika mwaka wa fedha 2016/17 programu hii ilitayarisha miongozo miwili **(2)** ya namna ya kupanga mpango wa mwaka wa Wizara na mpango wa Timu za Afya za Wilaya. Miongozo hiyo inatoa maelekezo ya jinsi ya kupanga mipango itakayoleta matokeo *Result Based Planning.*

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera ya Afya ya mwaka 2012 na Mpango Mkakati wa Tatu ambao utekelezaji wake ulianza mwaka 2013/14. Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo ilifanya mapitio ya Mpango huu, kwa lengo la kutathmini utekelezaji wa malengo na mikakati ya Wizara. Mapendekezo yaliyotolewa katika mapitio ya mpango huo yamesaidia kutayarisha vipaumbele vya sekta kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara imeanzisha utaratibu wa kupima utendaji kazi katika vituo vya afya na hospitali katika Wilaya za Unguja na Pemba. Kazi hii imefanyika kwa kutumia fomu maalumu iliyotayarishwa *Performance Assessment and Facility Rating Tool.* Kwa kutumia fomu hii maeneo yote ya utoaji wa huduma kama vile utawala, afya ya uzazi na mtoto, huduma za maradhi ya kuambukiza na yasiyoambukiza, afya ya mazingira, utunzaji na uhifadhi wa dawa na vifaa tiba pamoja na huduma nyenginezo, hufanyiwa uhakiki mara moja kwa mwaka. Katika uhakiki huu vituo vya afya hupatiwa nyota kuanzia moja hadi tano kulingana na utendaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, kazi hiyo ilianza kwa kutoa mafunzo kwa watendaji *Assessors* 32 kutoka katika vitengo mbali mbali pamoja na vituo vya afya. Jumla ya vituo 66 katika Wilaya nne (4) za Wete, Mjini, Kusini na Kati zilifanyiwa uhakiki. Katika matokeo ya uhakiki huo, vituo 31 vilipata nyota moja (1), vituo vinne (4) vilipata nyota mbili na vituo 31 havikupata hata nyota moja. Aidha, hakukuwa na kituo hata kimoja kilichopata nyota tatu (3), nne (4) au tano (5). Kadri nyota zinapokuwa nyingi, ndio inaonesha utendaji bora wa kituo. Hivyo, matokeo haya yameonesha kwamba bado tunahitaji kuimarisha utendaji wa vituo vya afya ili viweze kutoa huduma bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, program hii pia inashughulikia masuala ya kusimamia maadili ya tafiti za afya kupitia Kamati maalumu iliyoanzishwa *Zanzibar Medical Research Ethics Committee - ZAMREC.* Kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilipokea jumla ya maombi *Proposals* 21 ya kufanya tafiti za afya. Kati ya hayo, maombi sita (6) yalikubaliwa kuendelea na tafiti, maombi 12 yalirejeshwa kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho na maombi matatu (3) yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara ya Afya imeanzisha utaratibu wa kufanya kongamano la wadau wa tafiti za afya kwa lengo la kupata matokeo ya tafiti zilizofanywa, ili ziweze kutumika kwa ajili ya

kufanya maamuzi na kupanga mipango mbali mbali inayohusu Sekta ya Afya. Kongamano hilo litakuwa linafanyika kila mwaka; hivyo, Wizara inawaomba watafiti kutumia fursa hii kutangaza matokeo ya tafiti zao, ili yasaidie katika kutatua changamoto mbali mbali zinazoikabili jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mipango ya maendeleo ya sekta yeyote ile inategemea kuwepo kwa taarifa sahihi na zinazopatikana kwa wakati. Kitabu cha taarifa za afya *Health Information Bulletin* cha mwaka 2015 kimechapishwa na kusambazwa ili wahusika waweze kutumia taarifa hizo katika kupanga mipango yao. Kitabu hiki huwa kinatoa viashiria na taarifa mbali mbali zikiwemo za wagonjwa, magonjwa na huduma zinazotolewa katika hospitali na vituo vya afya vya Serikali na binafsi. Aidha, mafunzo mbali mbali ya ukusanyaji na uhifadhi wa taarifa za afya katika vituo vya afya vya Serikali na binafsi yalitolewa. Jumla ya wafanyakazi **66** walipatiwa mafunzo hayo, ambapo wafanyakazi 54 ni kutoka vituo vya afya vya Serikali na 12 kutoka katika vituo vya binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha matumizi ya takwimu, Wizara imo katika matayarisho ya kutengeneza mfumo wa ghala la taarifa za afya *HIS data ware- house*. Mfumo huu utasaidia kuhifadhi takwimu zote za afya kutoka vyanzo vya ndani *HMIS, ¡HRIS, LMIS* pamoja na taarifa zinazohusiana nazo kutoka vyanzo vyengine vya taarifa, ikiwemo taarifa za vizazi na vifo kutoka Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo na taarifa zinazotokana na Sensa ya Watu na Makaazi pamoja na tafiti za afya kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha jamii inapata taarifa sahihi juu ya mambo yanayotekelezwa na Serikali katika Sekta ya Afya. Wizara imeanzisha jarida maalum linalojulikana kwa jina la "Jarida la Afya". Jarida hili litakuwa linatolewa kila baada ya miezi sita (6) na kusambazwa kwa wananchi litakuwa na taarifa za matokeo ya Sekta ya Afya, yakiwemo mafanikio mbali mbali yanayopatikana kwa kipindi husika. Toleo Namba moja la jarida hilo lenye taarifa kuanzia mwezi wa Julai hadi Disemba, 2016 tayari limeshatolewa na kwa kusambazwa kwa wananchi. Jarida hili pia litatoa taaluma juu ya namna ya kujikinga na maradhi mbali mbali yanayoikabili jamii. Hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa ujumla walisome jarida hili, ili wafahamu mambo mbali mbali yanayohusiana na afya na yanayotekelezwa Wizara ya afya.

Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa malengo ya Wizara yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Utekelezaji wa majukumu hayo ni kama ilivyoelezwa katika Programu za Kinga, Tiba; na Sera na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Afisi ya Uratibu wa Shughuli za Afya Pemba ilitengewa jumla ya Shilingi 7,495,100,000 ambapo, kati ya hizo, Shilingi 6,515,600,000 ni kwa ajili ya mishahara na maposho ya wafanyakazi na Shilingi 979,500,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2017, jumla ya Shilingi 5,607,105,470 zimetumika, sawa na **asilimia** 74.8 ya fedha zilizotengwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kwenda kwenye maelezo muhimu utaniongeza dakika chache tu moja kwa moja kwenye changamoto kwa sababu ndio zinazotukabili, kwa hivyo programu hizi mbili zote naomba ziingie kwenye Hansard mpaka kifungu cha 150.

CHANGAMOTO

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya mafanikio yote hayo pia tuna changamoto lazima tuseme ukweli changamoto zipo na hasa katika sekta ya afya kwa sababu inagusa maisha ya wananchi wote wa Zanzibar moja kwa moja, inatugusa pia pamoja na maisha yetu sisi Wawakilishi wa wananchi tuliokuwemo humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yote hayo yaliyopatikana pia zipo changamoto, kulikuwa na changamoto mbali mbali ambazo ziliathiri utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2016/2017. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Ongezeko la idadi ya watu Zanzibar na idadi ya uzazi tunazaa sasa hivi kwa kasi kubwa sana tumevunja rikodi hatujawahi, wakati tunaandika kitabu hichi wastani wa watoto 72,000 lakini wakati nazungumza asubuhi hii tuko wastani wa 85,000 Zanzibar hivi karibuni kwa mwaka sisi tutakuwa tunaongezeka kwa laki

moja kwa sababu Mnazi Mmoja juzi tulivunja rikodi tulipata vizazi 100 kwa siku.

Hii inaonyesha kwamba wanaume wamebarikiwa na kina mama nao wamebarikiwa maana wengine wanatoka mayai mawili mawili kwa pamoja hili la kwanza ambayo ni changamoto yetu kubwa ambayo sote tunatakiwa tuwe pamoja katika kukabiliana nayo.

ii. Ongezeko halisi la mahitaji ya huduma za afya ukilinganisha na uwezo halisi wa fedha uliokuwepo kwa kugharamia kikamilifu huduma hizo; Hapa tunamshukuru sana Mhe. Rais katika *Priority* tuliyopewa ni mimi na Waziri wa Elimu bajeti zetu ndio zilizopewa *Priority* ya mwanzo tuliitwa na sisi ndio *Allocation* ya mwanzo ya fedha tulipewa, lakini bado kutokana na maongezeko hayo bado fedha hizi hazitoshi kwa sababu uhalisia umo katika ukusanyaji wa fedha zile.

iii. Uchakavu wa baadhi ya majengo kwa sababu mengi tumerithi tunamshukuru Dkt. Ali Mohammed Shein majengo mapya matatu ametufungulia mawili pale Mnazi Mmoja moja kule Abdalla Mzee, mengine yanaendelea kujengwa mtaona hivi karibuni na Hospitali ya Binguni inakuja Mwakani lakini bado kuna majengo ya zamani ambayo tunatumia la Kwanza ni Hospitali ya Mnazi Mmoja ambalo jengo la mwaka 1923 Jengo hilo ni la zamani mpaka njia zile za michirizi za maji zimeshazidiwa sasa hvi. Kwa sababu jengo lile limejengwa wakati Zanzibar ina *Population* ya watu laki tatu na thalathini elfu wakati huo.

Leo jengo lile ndio Hospitali yetu kuu inahudumia milioni 1.44 ya Wazanzibari ambao tunaendelea kuwa kwa laki moja karibu kila mwaka naamini sasa hivi tutakuwa tumeshapita milioni moja na laki tano.

Jengo la pili ni la Kidongo Chekundu ambalo limejengwa mwaka 1968 iliyopita pamoja na hospitali zetu za Chake Chake kule Pemba.

iv. Kushuka kwa kiwango cha chanjo kwa hapa Zanzibar sisi tulikusudia kufikia asilimia 90 lakini kuna sababu nyengine mbali

mbali ambazo hatukuweza kufikia asilimia 90 tumefikia asilimia 79 ile niliyoeleza. Lakini moja wapo ya sababu hiyo ni wananchi pia nao kutotupa mashirikiano, kuna *dreep* humu tunapigana wenyewe kwa wenyewe na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mnazijua kuna *dreep* za kisiasa kuna *dreep* za kudanganyana mambo ya nguvu haya na nini tunapeana huko kwa hivyo tunapata matatizo.

Hata katika hizi dawa za Malaria kuna *dreep* hivyo hivyo na nyie mnazijua sina haja ya kusema zaidi.

MWELEKEO WA BAJETI NA MALENGO YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo utanivumilia kwa sababu namalizia. Nia ya Serikali ni kutoa huduma bora za afya kwa wananchi, kama ilivyoainishwa katika Mikakati ya Kitaifa. Hivyo, naomba yaliyobakia yaingie kwenye *Hansard* nitakwenda moja kwa moja katika malengo ambayo tumejiwekea katika Program ya Huduma na Kinga na Elimu ya Afya 156, pamoja na Program ya huduma ya Hospitali ya Mnazi Mmoja 158 kwa malengo yetu tuliyojipangia mwaka huu naomba yaingie kwenye *Hansard* pamoja na Program ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya yaingie kwenye Hansard.

Wizara katika mwaka wa Fedha 2017/2018 imepanga kutekeleza shughuli zake ili kufikia malengo yaliyomo katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2020), Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini *MKUZA III*, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020, Sera ya Afya ya (2011) na Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliarifu Baraza lako kwamba kuanzia mwaka 2017/2018, huduma zote za afya ya msingi katika ngazi ya vituo zitahamishiwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ. Maamuzi haya yanatokana na kupitishwa kwa Sheria ya Ugatuzi Namba 7 ya mwaka 2014 na maamuzi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuhakikisha huduma hizi zinasimamiwa katika ngazi ya Halmashauri/Manispaa. Katika utaratibu huu, Wizara ya Afya itaendelea kutoa miongozo na ushauri wa kitaalamu, ili kuhakikisha huduma hizo zinapatikana katika ubora uliokusudiwa, na pia kufanya kazi kwa karibu na Wizara husika. Aidha, Wizara ya Afya itaendelea na jukumu la kutayarisha miongozo ya utoaji wa huduma za afya; kusimamia program za udhibiti wa maradhi mbali mbali;

kuratibu shughuli zinazohusiana na mfumo wa takwimu na taarifa za afya; na ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Uchangiaji wa huduma za Afya, Serikali imeshatowa maelekezo kuhusu maeneo ambayo yataruhusiwa kuchangiwa na yale ambayo hayatachangiwa na wananchi kwa mujibu wa sera na miongozo yetu. Hivyo, Wizara imeagizwa kuyafanyia tathmini ya kina mapato yanayotarajiwa kupatikana kutoka na uchangiaji pamoja na gharama za uendeshaji wa huduma ambazo hazitachangiwa. Kazi hiyo inaendelea na tunatarajia kuikamilisha mwanzoni mwa robo ya kwanza ya mwaka ujao wa fedha na kuiwasilisha katika vikao vya Serikali kwa kujadiliwa na hatimae kuridhiwa kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Wizara itaendelea kutekeleza malengo yake kwa kutumia mfumo wa bajeti ya programu, ambapo jumla ya programu kuu nne (4**)** zitaendelea kutekelezwa, nazo ni:-

i. Programu ya Kinga na Elimu ya Afya;
ii. Programu ya Tiba;
iii. Programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja; na
iv. Programu ya Usimamizi wa Sera na Utawala.

Programu ya Huduma za Kinga na Elimu ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa huduma za kinga za maradhi ya kuambukiza na yasioambukiza zinaimarika**,** Wizara imeweka malengo yafuatayo:-

i. Kuanzisha utoaji wa chanjo ya kinga ya Saratani ya Shingo ya Kizazi kwa wasichana walio na umri kuanzia miaka tisa (9);
ii. Kuimarisha huduma za mama na mtoto;
iii. Kuimarisha huduma za elimu ya afya;
iv. Kuimarisha huduma za afya katika skuli;
v. Kuimarisha huduma za kupambana na maradhi yasiyoambukiza ikiwemo uchunguzi wa kansa ya matiti, shingo ya uzazi na tezi dume;
vi. Kuimarisha “Kampeni ya Kumaliza Malaria Zanzibar” kwa kuongeza kasi ya kufuatilia wagonjwa wanaogundulika na maradhi hayo; na
vii. Kuendeleza mapambano dhidi ya maradhi ya kuambukiza, ikiwemo UKIMWI, Kifua Kikuu na Ukoma.

Programu ya Huduma za Tiba

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha upatikanaji wa dawa muhimu na huduma za uchunguzi na matibabu, Wizara imejipangia malengo yafuatayo:-

a. Kuimarisha upatikanaji wa dawa muhimu kwa mujibu wa muongozo uliopo *(essential medicines list)*, vifaa tiba, vitendanishi na vifaa vya uchunguzi wa huduma za mionzi *(Radiology);*
b. Kuimarisha mfumo wa rufaa wa wagonjwa katika ngazi tofauti;
c. Kununua vifaa vya uchunguzi (ikiwemo mashine ya DNA);
d. Kutayarisha Sheria ya Maabara;
e. Usimamia utekelezaji wa Sheria ya Chakula, dawa na Vipodozi; na
f. Kuimarisha huduma za tiba asili na tiba mbadala.

Programu ya huduma za Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Mwenyekiti, programu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja inahusika na usimamizi na uendeshaji wa hospitali, pamoja na kutoa huduma za uchunguzi na matibabu kwa wagonjwa, ikiwemo huduma za rufaa. Katika kufanikisha hili, program hii imejipangia malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto;
ii. Kuimarisha huduma za uchunguzi na matibabu;
iii. Kuwapatia mafunzo na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa hospitali katika fani mbali mbali ili kuimarisha ubora wa huduma za afya;
iv. Kufanya matengenezo ya miundo mbinu na ununuzi wa vifaa tiba;
v. Kuimarisha mafunzo ya vitendo yanayotolewa kwa wanafunzi wa kada mbali mbali; na
vi. Ujenzi wa wodi ya wagonjwa wa Akili katika Hospitali ya Kidongo Chekundu.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, katika programu hii Wizara imejipangia malengo yafuatayo:-

i. Kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Bima ya Afya Zanzibar;
ii. Kufanya mapitio ya mfuko wa fedha kwa Timu za Afya za Wilaya ili uendane na mpango wa ugatuzi wa madaraka;
iii. Kuendelea kuimarisha mfumo wa taarifa za afya na uibuaji wa tafiti za afya na zinazohusiana na afya;

iv. Kupitia na kutengeneza miongozo ya kisera ya utoaji wa huduma za afya;

v. Kuimarisha nguvu kazi kwa ajili ya Sekta ya Afya hususan kusomesha madaktari bingwa;

vi. Kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali ikiwemo Sheria ya kuendesha hospitali za binafsi na sheria ya madaktari;

vii. Kuanzisha rasmi zoezi la upimaji wa ufanisi wa wafanyakazi kwa ngazi zote Unguja na Pemba;

viii. Kuendelea kuratibu uimarishaji wa miundombinu ya afya ikiwemo:-

ix.

a) Kukamilisha ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

b) Kufanya ukarabati mkubwa wa jengo la huduma za macho;

c) Kujenga nyumba za madaktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee;

d) Kujenga jengo la wodi za watoto na wajawazito katika Hospitali za Kivunge na Makunduchi;

e) Kuanza matayarisho ya ujenzi wa Hospitali ya Binguni kwa kufanya uchambuzi yakinifu na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi huo;

f) Kufanya ukarabati wa Hospitali ya Chake Chake; na

g) Kuratibu ujenzi/matengenezo ya vituo vya afya 15 (Unguja 8 na Pemba 7) chini ya mpango wa ORIO Kiambatisho Namba 16 kinaonyesha vituo hivyo; na vinane (8) kupitia msaada wa Milele Foundation.

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Sekta ya Afya kwa mwaka 2016/2017 hayatokani na juhudi za Wizara ya Afya pekee, bali ni kwa mashirikiano na wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi. Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, Sekta binafsi, Washirika wa Maendeleo na wananchi wote kwa pamoja ambao walitoa michango yao ya fedha na utaalamu katika kuhakikisha malengo ya Sekta ya Afya yanafanikiwa. Wizara inawashukuru kwa moyo waliouonesha na tunawaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuimarisha huduma za afya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Shukrani za pekee ziende kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, ambao wametupa mchango mkubwa sana pamoja na ule mchango wa bilioni karibu thalathini na tatu za Hospitali ya Abdalla Mzee zote ni *grant* sio mkopo. Serikali ya Denmark, Uholanzi, Cuba, Canada, Israel, Norway, Misri, Ujerumani, Korea, Uturuki, India, Kuwait, Marekani, Italy, Saudi Arabia na Uingereza na wao hawakuwa nyuma katika kutuunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia muda wako ulionipa na muda wa Baraza lako tukufu naomba nielekee moja kwa moja kifungu cha 160 hivi sasa kuelezea

mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya afya kwa mwaka 2016/2017 hayatokani na juhidi za Wizara ya Afya pekee, bali ni kwa mashirikiano na wadau mbali mbali naomba nitoe neno la shukurani kwa wadau wetu mbali mbali ndani na nje ya nchi, Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali, sekta binafsi pamoja na washirika wa maendeleo na wananchi wote kwa pamoja ambao walitoa michango yao ya fedha, na utaalam wao katika kuhakikisha malengo ya sekta ya afya yanafanikiwa. Wizara inawashukuru kwa moyo wetu wote kwa moyo wao walioonyesha na tunawaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuimarisha huduma za afya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kutoa shukrani kwa watu binafsi kwa mtu mmoja mmoja; wa Kwanza kabisa ni Rais wangu Dk. Ali Mohammed Shein naomba nikiri amekuwa mstari wa mbele sana kunipa taaluma, kunipa elimu maana Wizara hii si nyepesi kila tunapokwama tukiwa tunakwenda kwa kiongozi wetu amekuwa mstari wa mbele sana kutupa miongozo ambayo imetusaidia na kutufanikisha kufika hapa leo tulipo sisi sote kwa pamoja.

Wa Pili ni Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa, Balozi Seif Ali Iddi kila panapotokea tatizo yeye anakuwa ni wa mwanzo kuwa pamoja na sisi bega kwa bega kutupa *supporter* yake hata kwenye kipindupindu basi tunakesha pamoja, yeye anatusaidia Mstari wa mbele kupigana na hichi kipindupindu tunachoendelea nacho.

Naomba nimkumbe sana mama yetu mpendwa Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mwanamwema Shein, mama yetu huyu hakutuacha mkono katika shughuli yetu yoyote ile iwe ja kijamii, iwe ya wauguzi, iwe ya madaktari, iwe ya kinamama, iwe ya afya, wajawazito yeye amekuwa pamoja nasi tunakushukuru sana mama Mwanamwema Shein.

Naomba tumshukuru Mke wa Makamu wa Pili wa Rais, Mama Asha Balozi nae amekuwa mstari wa mbele na kila panapotokea mapungufu hawi kama wengine wa kupiga mdomo yeye huja moja kwa moja na vifaa akatuchangia pale Mnazi Mmoja bila ya kusema, tunakuja sisi kusikia baadae kama mama Asha Balozi ameshachangia hilo na ameshaondoka, tunamshukuru sana.

Waheshimiwa Wawakilishi wote tunashuwakuruni kwa kujitolea kwa hali mali na michango yenu mbali mbali ya kushirikisana nasi katika shughuli mbali mbali za Wizara ya Afya, hatujasahau mmetusaidia katika kufanya usafi pia Hospitali ya Mnazi Mmoja, siku ya Mei Mosi wafanyakazi wanaadhimisha nyinyi mlijitolea kuja kufanya usafi pamoja nasi pale Hospitali ya Mnazi

Mmoja, hatujasahau hilo na tunakushukuruni sana Mheshimiwa kupitia kwako, pamoja na uongozi wa Baraza la Wawakilishi na wawakilishi wote.

Shukurani nyingine ziende kwa mashirika mbali mbali kwa misaada yao ya kifedha, kitaalamu na kiufundi wanayotupatia katika Wizara ya Afya, mashirika hayo ni; Shirika la Afya Ulimwenguni *(WHO), UNICEF, UNFPA, HAUKELAND UNIVERSITY HOSPITAL* ya *Norway, Neurosurgical Education Development* ya Spain wale wanaofanya upereshen za uti wa mgongo na ubongo mpaka sasa hawa wamejitolea kufanya upereshen 600 hapa Zanzibar kwa wananchi wa Zanzibar, watatu wakiwa wametokea nje ya Zaznzibar mmoja Dubai na mmoja Mombasa Kenya. *SAVE the CHILDREN, D-Tree International, Sight Saver, HIPZ, JHIEPIGO*, Mfuko wa Kupambana na UKIMWI, Ukoma, Kifua Kikuu na Malaria *(Global Fund to Fights AIDS, Tuberculosis & Malaria)*, Mfuko wa Rais wa Marekani *(PMI), DFID, Karolinska Institute, JHPU, IHI, WATER AID, Rotary UK, PEPFAR, ZOP, Zanzibar Milele Foundation, Muzdalifa Islamic Charitable Society*, Jumuiya ya Maendeleo ya Watu wa Pemba nao hawakuwa nyuma katika kutuchangia moja kwa moja hasa kule Micheweni tunakushukuruni sana, na wale wote ambao sikuweza kuwaorodhesha katika hotuba hii fupi sana ya kwangu naomba pia nao niwashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamaliza hotuba yangu naomba kuwashukuru wale wote waliochangia katika kutayarisha hotuba hii. Naomba shukurani zangu maalum ziwaendee Naibu Waziri wangu mpendwa, wa Afya Mheshimiwa Harusi Said Suleiman, Katibu Mkuu, Bi Asha Ali Abdulla ambae yupo pale juu anang'ara, Naibu Katibu Mkuu, Bi Halima Maulid Salum ambae nimekuja nae leo, Mkurugenzi Mkuu, Dr. Jamala Adam Taib, Afisa Mdhamini Pemba Bakar Ali Bakar, na Wakurugeni wote wa Idara mbali, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya na vitengo mbali mbali, watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kufanya kazi kwa juhudi kubwa sana, umakini na maarifa, ambayo yamenisaidia kufanya kazi na kutekeleza majukumu yangu kwa wepesi.

Aidha, shukurani za pekee ziende kwa Bi Attiye Mkurugenzi wangu wa Mipango ambae tumekesha mara kadhaa kwa ajili ya kutayarisha hotuba hii tukiwa pamoja, kushirikiana na Wakurugenzi wengine wote nawashukuru sana wamenipa moyo mkubwa sana. Aidha naomba niwashukuru wasaidizi wangu wawili amboa wanafanyakazi katika Ofisi yangu moja kwa moja Ndugu Septuu na ndugu Mwanaidi ambao wamekuwa mstari wa mbele kukesha hata pale tunapokuwa hatuna umeme wakati mwengine umezimwa basi tunafanya kazi kizani kwa kutumia mishumaa. Naomba niwashukuru wananchi wote wa

Zanzibar pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Kiembe Samaki ambao leo wameniwezesha kusimama hapa na kuweza kutoa hutuba hii mbele yenu.

Naomba pia nitoe Shukurani maalum na za Kipekee kwa wale mashujaa wetu Madaktari, Wauguzi na Wakunga pamoja na wasaidizi wao na ma-*orderly* ambao wamekuwa wakikesha na wagonjwa mbali mbali, na wakitumia muda mkubwa sana kuwahudumia wananchi wa Zanzibar. Malipo tunayolipa sisi na mishahara yao hayatoshi mbele ya malipo wanayolipwa na Mwenyezi Mungu *Subuhanahu wataala*. Mwenyezi Mungu ataendelea kuwalinda na kuwapa nguvu kubwa zaidi kuendelea kutoa huduma, kwa sababu huduma ya kutoa matibabu kwa wagonjwa ni huduma ya wito. Naomba niendelee kuwapongeza watumishi wengine wote waliokuweko katika hospitali zetu mbali mbali za vituo vya afya vyetu kuanzia vikubwa mpaka vile vidogo vya watu wawili vya kule Matemwe Kijini wanaotoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar.

.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, naomba Wajumbe wa Baraza lako waichangie hotuba hii, watushauri tuko tayari kupokea usahauri wao ipasavyo na hatimaye nawaomba kwa heshima na taadhima waidhinishe bajeti ya Wizara ya Afya ili kwenda kuwatumikia wananchi ambao wao wanawakilisha moja kwa moja matumizi yenyewe ni jumla ya Shilingi 79,936,229,000 kwa matumizi ya mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo, tutatumia Shilingi 14,300,000,000 kwa kazi za kawaida, Shilingi 22,673,962,000 kwa ajili ya mishahara na maposho, na Shilingi 533,400,000 ni ruzuku kutoka serikalini. Pia Wizara imepangiwa kutumia Shilingi 10,906,000,000 kwa kazi za maendeleo na Shilingi 24,522,867,000 ni ruzuku kutoka kwa washirika wa maendeleo hapa nataka nirejee tena wale wanaosema washirika wa maendeleo hawatuungi mkono Zanzibar kwa sababu nyengine yoyote wanayoijua wao si kweli, safari hii tumepanga nao pamoja bilioni 24.52 hii ni asilimia kubwa ya bajeti ya Wizara yetu (Viambatisho Namba 17 (a) na (b)).

Aidha, naomba Baraza liidhinishe matumizi ya Shilingi 10,380,579,000 kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kati ya hizo Shilingi 9,080,579,000 kwa ajili ya mshahara na maposho na Shilingi 1,300,000,000 zitatumika kwa mambo mbali mbali pamoja na lile paa linalovuja. Vile vile, naomba Mhe. Mwenyekiti Baraza lako liikubalie Wizara ya Afya ichangie Shilingi 221,143,000 kwenye Mfuko mkuu wa Serikali na Hospitali ya Mnazi Mmoja ichangie Shilingi 931,022,000 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti naomba niendelee kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa kunivumilia na kwa kunipa dakika za nyongeza za ziada kuweza kukamilisha hotuba yangu hii.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Wajumbe naomba sana kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya kwa hotuba yako fupi ambaye pia ni Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki. Sasa naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa jamii nae atoe Hotuba yake. Namuona Mhe. Viwe Khamis Abdalla kwa niaba ya Mwenyekiti.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii) Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kusoma Hotuba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara ya Afya ya mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, naanza hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kuniwezesha mimi pamoja na nyinyi Waheshimiwa Wajumbe kuwepo katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi wetu tukiwa wazima wa afya. Aidha natumia fursa hii kuwatakia wajumbe wote swaumu makbul na kwa uweza wake Mwenyezi Mungu na utukufu wa mwezi wa Ramadhani atujaalie kheri katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Waziri wa Afya Mheshimiwa Mahmoud Thabit Kombo, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kiembesamaki. Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Harusi Said Suleiman, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Wete na Katibu Mkuu Ndugu Asha Abdulla Ali, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Halima Salum Maulid na Watendaji wote wa Wizara ya Afya, kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusimamia sekta hii muhimu ya afya pamoja na changamoto zinazowakabili. Aidha, nawashukuru kwa kutupa ushirikiano katika kazi zetu za kuisimamia Wizara ya Afya. Kwa hakika lazima tuipongeze Wizara kwa kusimamia vyema suala la Afya ya wananchi wa Zanzibar katika Nyanja zote kinga na tiba.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii ina jukumu kubwa kikanuni kusimamia utekelezaji wa Shughuli za Serikali katika sekta ya Afya na Elimu, jukumu hili linafanyika kwa mashirikano makubwa ya Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ambao naomba kuwatambua kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini	Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Mjumbe
4. Mhe. Masoud Abdulrahman Masoud	Mjumbe
5. Mhe. Makame Said Juma	Mjumbe
6. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Mjumbe
7. Mhe. Hidaya Ali Makame	Mjumbe
9. Ndg. Aziza Waziri Kheir	Katibu
10. Ndg. Khamis Hamad Haji	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imepitia fungu H01 la Wizara ya Afya ambalo limejumuisha programu tatu. Kwanza ni Programu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya ambayo ina programu ndogo moja ya Kinga na Elimu ya Afya. Programu kuu ya pili ni ya Huduma za Tiba ambayo Programu zake ndogo ndogo ni ya Huduma za Matibabu na Huduma za Uchunguzi wa maabara na mionzi na Programu Kuu ya tatu ni Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya ambayo ina Programu Kuu ndogo za Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara na programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii pia imepitia fungu H02 la Hospitali ya Mnazimmoja ambalo linajumuisha programu mbili za Huduma za Uchunguzi na Matibabu na Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazimmoja.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi zake kubwa kuendeleza sekta ya afya ambayo katika kipindi chake cha Urais tumeona mabadiliko makubwa. Dkt. Ali Mohamed Shein anaendeleza kivitendo sera ya ASP na baadae CCM pamoja na malengo ya kuwapatia huduma bora za Afya Wazanzibari wote bila ya ubaguzi na malipo.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi wa kazi kubwa iliyofanyika katika Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba ambayo sasa ni Hospitali ya Mkoa, Kuimarishwa ujenzi wa Wodi mpya ya mama na watoto katika Hospitali kuu ya Mnazimmoja na mpango wa kuifanya Hospitali ya Mnazi mmoja kuwa Hospitali ya Rufaa unaendelea baada ya kupitishwa Sheria namba 3 ya mwaka 2016 ambayo imeanzisha upya muundo na uendeshaji wa Hospitali ya Mnazimmoja kama alivyofafanuwa Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake.

Mhe. Mwenyekiti, hayo ni machache kati ya mengi ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya katika Sekta ya afya ambayo muda hauruhusu kuyataja yote. Hata hivyo Kamati ya Ustawi wa Jamii inaendelea kuunga mkono juhudi hizo. Aidha kamati itakuwa tayari kuhakikisha mafanikio hayo yanaendelezwa na kudumishwa kwa kushauri na kuelekeza katika utekelezaji wake kwa mujibu wa Kanuni na sheria.

Mhe. Mwenyekiti, watu wenye afya bora ndio rasilimali kubwa ya nchi. Kwa mantiki hiyo Kamati yetu inapongeza sana Wizara ya Afya kwa kauli mbiu ya mwaka 2018/19 yenye kuendana na wakati inayosema "MWILI HUZEEKA, KADRI MTU ANAVYOZEEKA, BADILIKA, JALI AFYA YAKO".

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA KIBAJETI MWAKA WA FEDHA 2016/2017, NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/18

Mhe. Mwenyekiti, katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha unaomalizika wa 2016/17, Kamati ya Ustawi wa Jamii imepitia na kuona utekelezaji halisi wa majukumu waliyojipangia katika sekta mbali mbali za Afya. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Afya katika hotuba yake kwa mwaka 2016/17 Wizara hii iliidhinishiwa Shilingi bilioni 59.2. Hata hivyo, fedha zilizoingizwa kutoka hazina mpaka mwezi Machi 2017 ni shilingi bilioni 38.7, sawa na asilimia 65.6% ya fedha zilizotengwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mapato Hospitali ya Mnazimmoja ilipangiwa kukusanya shilingi bilioni 1.01. Hata hivyo hadi mwezi Machi 2017 jumla ya shilingi milioni 310 zimekusanywa sawa na asilimia 30.6%. Ingeafaa Mheshimiwa Waziri atujulishe ni sababu gani za msingi zilizopelekea kupatikana mapato machache nje ya matarajio.

PROGRAMU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Mhe. Mwenyekiti, Programu ya Kinga na Elimu ya Afya imeundwa kutokana na vitengo 12 vinavyotoa huduma mbali mbali za kinga na elimu ya Afya:

Kuimarisha huduma za uchunguzi wa maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza pamoja na kutoa elimu ya afya. Vile vile kuimarisha huduma za uzazi salama na kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi tatizo ambalo bado linaathiri jamii yetu. Kamati inaipongeza sana Wizara kwa kufanya upanuzi wa vituo sita ili viweze kutoa huduma za uzazi na watoto wachanga. Jambo la kupendeza zaidi ni kuhusisha upanuzi huo pamoja na uwekaji wa vitendea kazi

ikiwa ni pamoja na seti za kuzalishia, vitanda na majiko ya kuchemshia *(sterilizer).*

Mhe. Mwenyekiti, Progamu hiki ni muhimu sana kama nilivyotaja hapo awali ina vitengo 12. Fedha walizopatiwa kwa mwaka 2016/17 ni kidogo. Kiasi hicho cha fedha hakiakisi sana hali halisi ambayo Kamati ya Ustawi wa Jamii imekutana nayo wakati wa kufuatilia utekelezaji wake. Changamoto kubwa tulizozikuta katika utekelezaji wa Programu hii ni baadhi ya vituo kuendelea kuchangisha fedha katika huduma za uzazi. Hali hii inasababishwa na vituo hivyo kukosa vifaa muhimu vya kusaidia kinamama kama vile mipira, glavu, dawa na kadhalika ambazo zilitakiwa wapatiwe bila malipo lakini kutokana na uhaba wa fedha vituo vinalazimika kuwachangisha ili kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, Katika Makadirio ya mwaka 2017/18 Kamati ya Ustawi wa Jamii imeidhinisha jumla ya Shilingi bilioni 21.4 katika utekelezaji wa Programu ya Kinga na Elimu ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri kuwa katika utekelezaji kwa vitendo wa agizo la Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kutochangisha fedha katika huduma za uzazi, fedha hizo zilizoidhinishwa katika programu hii zifikishwe katika Hospitali na vituo vya afya ambavyo vinavyotoa huduma za uzazi na watoto kama zilivyokadiriwa tena kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukabiliana na maradhi ya Kuambukiza, bajeti ya mwaka huu 2017/18, kupitia programu ya Kinga na Elimu ya Afya, Wizara ilijielekeze zaidi katika kuweka mikakati inayotekelezeka ya kukinga maradhi badala ya kusubiri maradhi ya milipuko yatokanayo na kuchukua hatua. Mfano hai ni kuripuka kwa maradhi ya Kipindupindu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inasisitiza kuwa zoezi la kukinga kuibuka kwa maradhi haya, liwe endelevu kwa kuhakikisha elimu ya afya inatolewa kudhibiti uchafu katika maeneo mbali mbali yakiwemo yanayouzwa vyakula. Lakini kubwa zaidi ni baadhi ya mitaa katika Mkoa wa Mjini Magharibi watu wake kutotumia vyoo. Kamati inasikitishwa kwa habari kwamba tayari mripuko wa Kipindupindu umeshatokea tena kutoka mitaa ile ile ya kila siku. Kamati inaishauri Wizara ya Afya kila mara iwe inafanya operesheni maalumu za ukaguzi wa maeneo hayo kubaini nyumba zisizo na vyoo na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria na Kanuni za sheria ya Afya ya Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, maradhi yasiyoambukiza *(NCD)* nayo yamekuwa yakichangia athari za kiafya kwa wananchi wetu. Kamati inashauri Wizara ya Afya, kutumia kasma iliyoidhinishwa katika bajeti ya mwaka 2017/18, kupitia progamu hii, kuongeza utoaji wa elimu ya afya kwa wananchi hasa kupita shule za msingi, sekondari na vyuo na kuzidisha hamasa kwa wananchi kushiriki kufanya mazoezi. Kamati ya Ustawi wa Jamii inashauri Serikali kutoa fursa au wasaa maalumu kwa wafanyakazi wote wa Serikali kutumia angalau saa moja katika kila wiki kushiriki mazoezi ili kuimarisha afya zao. Aidha, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaishauri Serikali kuweka sheria au kanuni kali za kuyalinda maeneo ya wazi yenye viwanja vya kufanyia mazoezi nchini, yasivamiwe kwa shughuli za ujenzi wa makaazi na maduka ya biashara na badala yake maeneo hayo yabakie kutumika kwa shughuli za michezo ili kuimarisha afya za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kukinga uingiaji maradhi nchini ni muhimu sana kwa usalama wa afya za wananchi na nchi yetu. Kama tujuavyo kumekuwa na miripuko ya maradhi hatari katika maeneo mbali mbali duniani kama vile ebola, zika, mafua ya ndege, homa ya Dengue na kadhalika ambayo yanaenezwa na kuambukizwa kwa njia tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii imeona ni vyema kuishauri Wizara kufanya juhudi za makusudi kukiimarisha kitengo cha Afya cha Bandarini na Uwanja wa Ndege wa Abeid Aman Abeid Karume (AAAK) kiwe katika kiwango cha kimataifa katika kudhibiti uingiaji wa watu wenye maradhi nchini.

Mhe. Mwenyekiti, katika programu ndogo ya Kinga na Elimu ya Afya, huduma za afya bandarini zimekadiriwa kiasi cha shilingi milioni 20. Kamati ya Ustawi wa Jamii inapata wasiwasi kidogo kuona kama kiasi hicho cha fedha kilichokadiriwa kinaweza kuimarisha huduma za afya katika bandari zetu za baharini na anga. Kamati ya Ustawi wa Jamii imepata fursa ya kukaguwa shughuli za Kitengo cha afya Bandarini na Uwanja wa Ndege wa wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume, Kamati imebaini changamoto ambazo zinahitaji fedha zaidi ili ziweze kutatuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha afya katika bandari ya Malindi hakina eneo la uhakika la kufanya kazi zake. Kituo hakina Ofisi ya kudumu katika Bandari hiyo. Kamati imefamishwa kuwa uongozi wa Kituo umeomba nafasi ya kujenga kituo katika bandari hiyo lakini haikuwezekana. Kamati ya Ustawi wa Jamii inaishauri Serikali kupitia bajeti hii, kufanya haraka kujengwa kituo cha afya katika bandari ya abiria ili kazi ya usimamizi ki-afya kwa uingiaji na

utokaji wa watu nchini unakwenda kwa uangalifu mkubwa kukinga kuingia maradhi mapya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inaishauri Serikali kuwa wakati tunasubiri shughuli za afya kuhamia jengo jipya la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar (Abeid Aman Karume), tusisahau kutatuwa changamoto zilizopo sasa katika kitengo cha afya kilichopo hapo na Bandarini Malindi kupatiwa vifaa ambavyo baadhi vimeharibika.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mwenyezi Mungu atulinde na majanga makubwa ya maradhi katika nchi yetu, lakini tunalazimika kuchukua hatua ya kujikinga kwani gharama ya kudhibiti wakati yakitokea ni kubwa na nchi yetu inaweza kupata hasara kubwa katika kukabiliana nayo.

PROGRAMU YA TIBA

Mhe. Mwenyekiti, programu ya tiba ni muhimu sana kufanikisha lengo la kikabiliana na maradhi kwa wananchi. Mwaka wa fedha unaomalizika wa 2016/17, programu hii iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 11.2. Hadi Machi 2017 Wizara ilikwishapatiwa shilingi bilioni 10.9 sawa na 97.8%.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii imefuatilia utekelezaji wa programu ya tiba kwa mwaka wa fedha 2016/17 na imeona hatua mbali mbali za mafanikio katika utekelezaji wake. Kamati ya Ustawi wa Jamii imeridhishwa na juhudi za ununuzi wa dawa muhimu, vifaa tiba, vitendanishi na vifaa vya uchunguzi wa maabara. Kwa mwaka huu wa fedha unaomalizika, hali ya upatikanaji wa dawa katika Hospitali na vituo vyetu vya afya ilikuwa ya kuridhisha licha ya changamoto za hapa na pale ambazo zinaendelea kupatiwa ufumbuzi na Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Katika programu hii, Kamati ya Ustawi wa Jamii imeguswa sana na kusita kwa mpango wa ujenzi wa Bohari ya Dawa kisiwani Pemba ambao ulikuwa unadhaminiwa na Serikali ya Marekani kupitia *USAID* na hivi sasa udhamini huo umesita baada ya mabadiliko ya Serikali ya Marekani. Hata hivyo Shirika la Misaada la Marekani limeshatangaza kuendelea tena na mpango wake wa kusaidia Zanzibar. Hivyo tunaiomba Wizara ya Afya kuanza tena mazungumzo na Taasisi kufanikisha suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inatambua juhudi za Serikali za kutafuta fedha za kuendelea na mradi huo, hata hivyo, Kamati inashauri kupitia

programu hii, zitengwe fedha angalau za kuanza na ujenzi katika hatua za mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inapongeza hatua ya Serikali katika bajeti ya mwaka huu wa 2017/18 kutenga kiasi cha shilingi bilioni 1.8 katika mradi wa kukamilisha ujenzi wa jengo la Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar. Kamati inasisitiza sana fedha hizo zipatikane ili mradi huo ukamilike na kazi za Mkemia Mkuu zifanyike katika mazingira ya kuleta ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii ilitembelea jengo analofanyia kazi Mkemia Mkuu ambalo ni finyu na halipo katika mazingira mazuri ya kazi za Mkemia. Hivyo, fursa hii ya kibajeti itasaidia kuifanya Ofisi ya Mkemia Mkuu kuwa ya Kisasa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika programu ndogo ya Huduma za Matibabu, Kamati ya Ustawi wa Jamii imetazama katika kijifungu chenye kasma ya huduma za Hospitali za vijiji, Wilaya na hospitali za Rufaa ambapo katika bajeti ya mwaka huu 2017/18 kimekasimiwa shilingi bilioni 15.86. Kamati ya Ustawi wa Jamii baada ya ziara ya kupitia vituo kadhaa vya afya vya vijijini, wilaya na hospitali, tumeona changamoto mbali mbali ambazo tumejadiliana na Wizara namna ya kuzifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu kubwa ya changamoto hizo zinahitaji mipango na fedha ya kuzitatua. Kamati ya Ustawi wa Jamii inashauri serikali kuchukua hatua za makusudi na za dharura kuviimarisha vituo vya afya vya vijijini kwa kuvifanyia ukarabati wa miundombinu na kuvipatia wataalamu na vitendea kazi. Ni kwa kuboresha huduma katika vituo vya vijijini na Wilayani ndipo Wizara itapoweza kupunguza msongamano mkubwa unaotokea katika Hospitali ya rufaa ya Mnazimmoja na Hospitali nyengine za Mikoa.

Kamati ya Ustawi wa Jamii pia inaishauri serikali kuwa na utaratibu wa kuongeza bajeti ya kuimarisha vituo hivi vya afya kila mwaka ili kuviongezea uwezo wa kutoa huduma zaidi kwa wananchi hasa kwa akina mama na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, nachukua fursa hii kumpongeza Mrajis wa Bodi hiyo Dkt. Burhan Othman Simai kwa kazi anayofanya kwa uadilifu na uaminifu mkubwa kuhakikisha kuwa Bodi hiyo inafanyakazi zake kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, ni hivi karibuni tu ambapo Baraza hili lilifanya marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi na kuifanya kuwa Wakala unaojitegemea kwa baadhi ya kazi zake, hivyo kuiongezea ufanisi zaidi. Tayari sheria hii imeshaanza kutumika na ni matumaini yetu kuwa Sheria hiyo itaimarisha kazi za Uchunguzi wa Dawa, Vyakula na Vipodozi kwa madhumuni ya kulinda afya za wananchi wetu. Tunaipongeza sana Bodi kwa kurekebisha utaratibu mzima wa uchinjaji, ukaguzi na usafirishaji wa nyama ya ng'ombe na mbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inawaomba viongozi na wananchi kutoa ushirikiano kwa Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kuwa kumekuwa na dhana katika jamii yetu kuwa baadhi ya vyakula tunavyotumia vinahatarisha afya zetu. Kwa hivyo, Kamati ya Ustawi wa Jamii inachukua fursa hii kuwaomba wananchi washirikiane kutoa taarifa kwa Bodi kuhusu mfanyabiashara yoyote atakayeingiza chakula, dawa au vipodozi visivyokaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia programu hii ndogo ya Huduma za Uchunguzi Kamati ya Ustawi wa Jamii inaishauri Serikali kuingiza fedha zilizokasimiwa ili Bodi iweze kufanyakazi za kulinda afya za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika Programu hii ya Tiba, kuna huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala ambazo kwa mujibu wa maelezo ya hotuba ya Mhe. Waziri, Baraza limeweza kuongeza idadi ya waganga waliosajiliwa kwa mujibu wa taratibu, aidha Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala limetayarisha muongozo wa watabibu wa tiba asili juu ya kufanya vipindi katika vyombo vya habari. Kamati ya Ustawi wa Jamii inaipongeza hatua hiyo ambayo itasaidia kuweka udhibiti wa matangazo holela ya tiba asili na tiba mbadala.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii, inaendelea kuishauri kwa mara nyengine tena Wizara kufanya operesheni maalumu ya ukaguzi wa maeneo yasiyo rasmi ambayo yanatolewa huduma ya tiba asili na mbadala. Katika kipindi cha hivi karibuni kumetokea baadhi ya watu wanaotoa huduma za tiba asili na mbadala katika maeneo mbali mbali yasiyo rasmi kama vile sehemu za ibada, barabarani na sokoni bila kufuata utaratibu na wakati mwengine huduma wanazotoa hazijasajiliwa wala kufanyiwa ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inashauri Baraza lipewe ulinzi maalumu katika kufanya operesheni ukaguzi wa huduma za tiba asili na mbadala kwa madhumuni ya kuwabaini wale wote wanaotoa huduma hizo kinyume na utaratibu wa sheria.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Afya

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii imefanyakazi pia ya kupitia programu hii iliyokasimiwa shilingi bilioni 18.3 kwa mwaka wa fedha 2017/18. Katika programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara Kamati ya Ustawi wa Jamii imefurahishwa sana na azma ya Serikali kutenga fedha za kukamilisha mpango wa uanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar. Hili ni jambo jema na nachukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kukidhi kiu kubwa ya wananchi wa Zanzibar hasa wafanyakazi wa sekta ya umma kuweza kufaidika na huduma za Bima ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inashauri fedha zilizotengwa kiasi cha shilingi bilioni 2.2 katika bajeti hii zipatikane ili mpango huu uanze mapema iwezekanavyo ikiwemo kutungwa sheria ya kuanzishwa mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar. Kamati ya Ustawi wa Jamii inaiomba sana Serikali kuidhinisha fedha hizi katika bajeti hii kwa wakati kwani ni muda mrefu sasa wafanyakazi wa sekta ya umma wamekuwa na kilio cha kupata huduma za bima ya afya. Kamati ya Ustawi wa Jamii itafuatilia hatua kwa hatua kuanzishwa mfuko huu ambao mbali na kusaidia wafanyakazi pia unategemewa kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa huduma bora za afya katika hospitali zetu.

Programu ya Hospitali ya Mnazimmoja (H02)

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazimmoja ambayo hivi sasa ni Taasisi inayojitegemea kwa mujibu wa sheria namba 3 ya mwaka 2016, imekuwa na fungu lake ambalo ni H02 lenye Programu ndogo mbili:-

1. Programu ndogo ya kwanza ni Huduma za Uchunguzi na Matibabu,
2. Programu ndogo ya Pili ni ya Uendeshaji na Uratibu wa Hospitali ya Mnazimmoja.

Mhe. Mwenyekiti, Kitaasisi hospitali ya Mnazimmoja inajumuisha Hospitali ya Mwembeladu na Hospitali ya wagonjwa wa afya ya akili ya Kidongo chekundu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa za kuimarisha huduma za afya katika Hospitali ya Mnazimmoja kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake hivi punde, Kamati ya Ustawi wa Jamii imeona ni vyema Serikali

ikasikiliza na kuyazingatia maoni mengi ya wananchi wanaokwenda hospitalini hapo kama wagonjwa au wapokwenda kukagua na pia kuwapeleka wagonjwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imezigawa changamoto za Mnazimmoja sehemu mbili. Zile zinazogusa Serikali Kuu hasa upatikanaji wa fedha walizokisiwa kwa ununuzi wa dawa, vitendea kazi na kuwadhibiti wafanyakazi hasa madaktari na wafanyakazi kwa kuwapatia vivutio katika maslahi yao. Vile vile zipo changamoto za uongozi wa usimamizi wa Hospitali yenyewe. Wafanyakazi kuwajibika ipasavyo, si vyema Daktari kumwambia mgonjwa "njoo Hospitali yangu binafsi mathalan pale Machomane au Jang'ombe upate huduma ya *'ultra sound'* nzuri.

Pia suala la huduma ya usafi lugha nzuri kwa wagonjwa. Hivi Wizara imefanya utafiti kuona kwamba kiwango cha uuguzi (*nursing*) kimeporomoka sana mpaka kuwafanya wagonjwa kulala na jamaa zao ili wawasaidie hasa nyakati za usiku.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazimmoja inategemewa kuanza kutoa huduma za kusafisha figo ambazo ni gharama zake ni kubwa, Kamati ya Ustawi wa Jamii inashauri sana serikali kuhakikisha inajipanga kwa kutenga bajeti ya kutosha ya kufanya huduma hizo, kutayarisha vifaa na wataalamu ili huduma hiyo itolewe kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati kamati ya Ustawi wa Jamii ilipotembelea Global na Hospitali ya Muhimbili na kuona namna huduma ya kusafisha figo inavyotolewa, tumeona tushauri kwa dhati Serikali yetu kuwa mkakati wa kuanza huduma hiyo katika Hospitali ya Mnazimmoja ni muhimu uanze haraka na serikali iwekeze vya kutosha katika kufanikisha huduma hiyo ili iwe endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo kamati yangu imejifunza katika ziara yake katika Hospitali ya Muhimbili, ni namna Hospitali hiyo inavyowekeza katika rasilimali watu. Wataalamu wengi mabingwa wa fani mbali mbali wanapatiwa fursa za kujiendeleza katika fani na maarifa mapya na kisasa ya kitabibu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii imeona ni vyema ikashauri Serikali izingatie kuwekeza katika kupata wataalamu mabingwa wa fani mbali mbali za kitabibu, kwani kinachofanya Hospitali kuwa ya rufaa siyo majengo peke yake bali uwepo wa wataalamu bingwa wa magonjwa mbali mbali pamoja na vitendea kazi vya kutosha. Ni vyema malengo ya bajeti zetu yakakisi

shabaha za serikali kuwa na Hospitali ya Rufaa yenye wataalamu waliobobea na vifaa kwa kuwekeza katika taaluma zao na kununua vifaa vya kufanyia kazi.

Hospitali ya Mwembeladu

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mwembeladu bado ni muhimu katika kutoa huduma za uzazi, mama na watoto. Zipo baadhi ya changamoto za kibajeti katika hospitali hiyo ambazo Wizara imezifanyia kazi kama vile matengenezo ya mashine ya kufulia, Kamati inapongeza kwa hilo. Hata hivyo, bado kuna changamoto ya wauguzi kupatiwa sare na hili Kamati inaikumbusha Wizara kuweka kasma katika bajeti ili wauguzi wapatiwe fedha za sare kama wanavyopatiwa wafanyakazi wa taasisi nyengine za Serikali.

Mhe. Mwenyekitu, Kamati pia inaikumbusha Wizara kuongezea motisha na vivutio wauguzi wasimamizi *(nurse incharge)* ambao wanafanyakazi kubwa, sambamba na wauguzi wote kadiri hali ya bajeti inavyoruhusu. Hata hivyo, Kamati ya Ustawi wa Jamii inachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuongeza maslahi kwa watumishi wa umma wote wakiwemo wauguzi.

Hospitali ya Kidongochekundu

Mhe. Mwenyekiti, hali ya Hospitali ya wagonjwa wa afya ya akili ya Kidongo Chekundu bado ni changamoto kwa baadhi ya maeneo hasa ya vyoo na ukuta wa uzio. Kamati inashauri sana bajeti ya mwaka huu 2017/18 itumike kufanya ukarabati wa vyoo katika Hospitali ile ili kuwaepusha wagonjwa na majanga ya milipuko ya maradhi ambayo yanaweza kutokea kutokana na hali isiyoridhisha ya usafi. Suala la upatikanaji wa maji muda wote kwa saa 24 ni muhimu kuzingatiwa kwa undani zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Ustawi wa Jamii inakumbusha Wizara kuhusu kuongeza watendaji hasa wahudumu katika Hospitali ya Kidongo Chekundu, hili halihitaji bajeti bali mipango ya ndani ya Wizara yenyewe. Kuna Wauguzi wasiopungua 14 hospitalini hapo lakini cha ajabu wanafanyakazi wodini ni watano tu (5). Wauguzi wengi wa hapo hawataki kuingia zamu za jioni na usiku kwa sababu zisizo na msingi utawala unawaachia tu.

Mwisho

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru watendaji wa Wizara ya Afya wa Unguja na Pemba, wakiongozwa na Katibu Mkuu wao, Naibu Katibu Mkuu, Afisi Mdhamini Pemba na wakuu wote idara, taasisi na

vitengo vya Wizara. Tunawashukuru kwa mashirikiano yao wakati wote kamati ikifanya kazi zake pamoja nao.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii tena kuwashukuru wewe kwa kuiwezesha kamati ya Ustawi wa Jamii kufanya kazi na ziara mbali mbali katika kujifunza na kujiongezea maarifa, kwa lengo la kusaidia Wizara na Serikali kwa jumla. Aidha kamati inaishukuru Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza na Watendaji wake kwa mashirikiano na kuisaidia kamati kutimiza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nawashukuru wajumbe wa Baraza kwa umakini wao wa kutafakari hoja na kunisikiliza kwa utulivu mkubwa wakati wote nikiwasilisha hotuba hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru, na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha hotuba yangu ya Kamati naomba uniruhusu japo dakika tano kuchangia hotuba hii kwa kutoa mchango wangu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Viwe Khamis Abdalla, kwa hotuba yako na kwa uwasilishaji wako mzuri kwa niaba ya Mwenyekiti wa Ustawi wa Jamii nimekuruhusu kwa hizo dakika tano.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri na Watendaji wake wote kwa hotuba yao nzuri walioyotuletea na pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu utaanza kwenye Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya afya. Kwenye kitengo hichi kuna vituo vya afya ambavyo ni vipya vitajengwa hivi karibuni. Mhe. Waziri wa Afya nilimuuliza swali langu na yeye mwenyewe alinijibu ndani ya Baraza hili tukufu kwamba kituo kile kimeshakaa kwa muda mrefu na katika majibu yake akasema kuwa kituo kile kitafanyiwa kazi kwenye mwaka huu wa bajeti kwa kupitia wafadhili wa MILELE *Foundation*.

Mhe. Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha katika kitabu chake cha bajeti sikukiona, nimeona baadhi ya vituo vyengine tu. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake anipatie maelezo ni sababu gani ambazo kuwa zimepelekea wakati Barazani alinijibu kuwa kituo kile tayari

kimo kwenye bajeti yao ya mwaka huu lakini kwenye kitabu sikukiona. Namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo ya kutosha ili na mimi nipate kuunga mkono hotuba yake hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye chanjo za watoto. Hivi karibuni nilikwenda kwenye Hospitali ya Mnazimmoja nilipokwenda nilifika katika kitengo cha watoto wachanga nilisikia dokta akisema kama sasa hivi hatuna chango huu ni mwezi wa watatu katika kitengo hiki cha Hospitali ya Mnazi mmoja hakuna huduma ya chanjo. Mama yule aliyemleta mtoto wake alimuliza ni lini huduma hii itarejea Dokta alimjibu mama kama huduma hii hatujui itarejea lini. Kwa vile mimi ni mjumbe wa Kamati naomba Mhe. Waziri atapokuja anieleze ni sababu zipi ambazo zilipelekea huduma hii ya chanjo kwa watoto wachanga zikawa hazipatikani katika hospitali ile ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, nimalize na mchango wangu na ujenzi wa jengo la kupumzikia kwa wageni na wagonjwa wetu wakati wakifika pale hospitali ya Mnazi mmoja tulisikia kama kuna sehemu ambayo inataka kujengwa eneo kwa wale ambao wanakwenda pale wakisubiri muda wa kuangalia wagonjwa, lakini mpaka leo jengo hili bado halijaanzishwa nini hasa ambacho kimezuiya jengo hili lisianzishwe.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache nakushukuru sana kwa kunipa muda huu naunga mkono hotuba hii ya bajeti ya kamati yangu asilimia 95 asilimia 5 namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anipatie majibu ya kutosha na nitazuia fungu natoa azma yangu ya kuzuwia fungu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nami nakushukuru Mhe. Viwe Khamis Abdalla kwa uwasilishaji wako na kutoa mapendekezo yako binafsi kama ulivyosema waheshimiwa wajumbe hayo yalikuwa mapendekezo yake binafsi lakini maoni ya kamati yameunga mkono yameunga mkono asilimia mia lakini kwa mapendekezo yake binafsi amesema anaunga mkono asilimia tisini na tano mpaka waziri atakapoleta majibu ni haki yake ile ilikuwa maoni ya kamati hayo maoni yake binafsi kwa hivyo Mhe. Waziri utakapokuja Mhe. Viwe umpe majibu sahihi.

Waheshimiwa wajumbe tunaendelea lakini naomba kabla ya kuendelea niwakumbushe hii wizara imepata wachangiaji wengi sana, sasa nilikuwa nawaomba waheshimiwa wajumbe nitapomtaja mtu aende moja kwa moja katika mchango wake na ile azma yake,kuliko tukianza maelezo mengi mwisho wa siku dakika zako ishirini zinaisha utanambia Mwenyekiti niongeze dakika tano niongeze mbili. Kwa hiyo nawaomba sana waheshimiwa wajumbe twende

kwa misingi hiyo dakika zako ishirini uzitumie ipasavyo, kwasababu utapoanza shukrani na hekima na nini mimi nahesabu kuwa umeshanza kuzitumia zile dakika zako.

Kwa hivyo mchangiaji wetu wa mwanzo kwa siku yetu ya leo naomba nimwite Mhe. Suleiman Shihata wa Jimbo la Kijitoupele, atafuatiwa na Mhe. Mwantatu na kama muda upo basi nitampa nafasi Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuipata nafasi hii ya mwanzo kabisa kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya kwa bajeti yake ya mwaka 2017/2018.

Lakini pia Mheshimiwa nikupongeze wewe kwa kunipa nafas hiyo nampongeza pia Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Madaktari wetu na wauguzi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na matatizo ya hapa na pale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwanza hasa tukizingatia kwamba Mheshimiwa wetu katokea katika taasisi hii kwa hivyo fani yako kama wewe hapo mheshimiwa mwalimu na wewe na wewe utatizama umuhimu wako wa kazi ile ulotokea na lazima upongezwe au ipongeze taasisi yako.

Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kazi nzuri aliyoifanya katika nchi hii nikurudisha hadhi na matarajio ya wananchi wetu juu ya hospitali zetu za Unguja na Pemba lakini kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti pamoja na uzuri wa hospitali yetu ya Mwembeladu na ukienda Pemba Abdalla Mzee kuna mambo tofauti kidogo yanajitokeza naiomba wizara iyapokee na iyafanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi mmoja ni hospitali mama na Wazanzibari wote wanajua hapo ndio kimbilio lao la mwisho katika kutafuta afya zao lakini kwa mshangao na bahati mbaya iliyojitokeza kuna watendaji wao baadhi ya watendaji sio wote kama madaktari, wauguzi au nani lakini baadhi huwa hawafanyi kazi zao ipasavyo.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, kuna mgonjwa fulani alinijia juzi mimi kaenda hospitali ya mnazi mmoja kenda sehemu ya *X-Ray* kufika anambiwa *X-Ray* ile mbovu haifanyi kazi. Kwa bahati nzuri akatokea mgonjwa mwengine yule mshughulikiaji wa pale anajuana naye akamfanyia kazi ile, inaonesha dhahiri kwamba wananchi wetu mahitaji yao hawayapati kikamilifu namuomba Mhe.

Waziri watendaji wetu baadhi katika hospitali zetu hawafanyi kazi zao ipasavyo na hawana huruma na viapo vyao walivyokula, kwa sababu daktari au muuguzi anakula kiapo maalum kwa fani ile kama mwanajeshi. Askari yeyote anakula kiapo kwa kazi yake hata na sisi Wawakilishi hapa namuomba sana Mhe. Waziri hili waliangalie manung'uniko ya wananchi wetu wanyonge yamekuwa makubwa sana katika nchi yetu. Ukweli bila ya kuficha hospitali nzuri lakini matatizo mengi yanajitokeza kutokana na watendaji wake si waaminifu na hawana imani na wananchi wetu sio wote nasema tena baadhi yao.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi mmoja ni hospitali kuu nasema tunaitegemea na imeingizwa katika hospitali ya rufaa nimepata bahati ya kuitembelea na huwezi kwenda katika bajeti bila wizara unayoigusa kufainyia utafiti na kutembelea baadhi ya maeneo, hospitali Mheshimiwa inasikitisha sana ndani nimekwenda ghorofa ya tatu na ya pili Mheshimiwa hospitali vyoo vichafu, vimefurika uchafu na hatari hata kuelezea katika Baraza hili saa hizi watu wamefunga. Namuomba sana Mhe. Waziri hili waliangalie na liko nje halitaki tochi vyoo vichafu vimefurika uchafu nafikiri kiswahili kimefahamika.

Lakini jengine Mheshimiwa nilipata bahati ya kutembelea Chumba cha Muuguzi ghorofa ya tatu ofisi ile inavuja inashangaza kidogo sasa ningemuomba Mhe. Waziri yeye na Naibu Waziri na Watendaji wake, Katibu nani wako mbali lakini uaminifu kile chumba alokabidhiwa yule muhusika ajuwe uhakiki wa kazi zake au uhakika wa kazi zake hapa inadhihirisha wazi kwamba umepewa nafasi hii kashughukie pahali fulani lakini muda hana. Mhe. Waziri haya tunayoyasema yako nje na wananchi wameyashuhudia na mimi mmoja nasema hii kama mwezi wa Ramadhani nimefunga swaumu yangu kesho ndio amali yangu kwa Mwenyezi Mungu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nakwenda katika hospitali hizi kwa ufupi sana Hospitali ya Wete nilipata bahati ya kwenda kutembelea hospitali hii kama Mwakilishi nina haki ya kwenda popote bahati mbaya au bahati nzuri naweza kusema mbaya kuna kitengo cha nusu kaputi hapa Mhe. Mwenyekiti, hii ni sehemu muhimu lakini kuna mfanyakazi mmoja baada ya kumuuliza mama huyu yeye anakaa Mchanga mdogo gari la kuchukulia wagonjwa likitoa tatizo akachukuliwe yeye zaidi ya tatu au nne au sita kwa siku pindi linapotokea kwa hivyo hii inaonyesha dhahiri bado pana matatizo na lipatiwe ufumbuzi. Ufumbuzi wenyewe ni kama huu ufuatao pana nyumba ya madaktari pale au ya wauguzi lakini wanakaa watu wasiohusika. Kwa hivyo mimi ninamshauri sana Mhe. Waziri huyu mama akatafutiwa nyumba kuishi pale ili awe karibu na

hospitali ile kwa sababu maradhi yanapotoke hayana wakati, wakati wowote inapotokea inakuwa ni maradhi yanotaka kupata kutibiwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nilishuhudia katika Uongozi wa Pemba katika Wizara ya Afya hakuna mwanamke hata mmoja katika Kamati ya Uongozi sasa jinsia tunasema tusiwe mbali kuna mambo mengine ya kinamama wanajuana wenyewe, ningemuomba Mhe. Waziri na hili waliangaliye mimi hasa nazungumzia hili kwasababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake na Watoto. Kwa hivyo naomba tu Kamati hii ya Uongozi Wizara ya Afya Pemba ilingalie hili ni suala kubwa kwamba hamna mama hata mmoja, kwa hivyo ni upendeleo Mheshimiwa uangaliwe wapatiwe kazi ambayo inawasaidia.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti kuna Hospitali ya Abdalla Mzee ni nzuri sana wazee wetu walisema historia inajirudia lakini kujirudia kwenyewe kwa vyengine ilivyojengwa na ilivyobadilika ni historia tosha kwamba imerudi katika hali nzuri zaidi kuliko ilikotoka. Lakini bahati mbaya, kuna kitengo cha yaani mashine ya kuchomea taka hivi sasa hivi ni mbovu Mheshimiwa ni mbovu naomba tuu Mheshimiwa uliangalie kwasababu pana mataka mengi pale tumeyaona naomba sana Mheshimiwa hili ulitafutie dawa liondokea kwa sababu hospitali nzuri jambo hilo linatengenezeka liondoke tatizo hilo.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, mimi nina ombi maalum kwa upande wangu nawapongeza sana hospitali binafsi nawapongeza kwa kazi zao nzuri, nawapongeza wanapo wapokea wananchi yaani wagonjwa lakini la kusikitisha madaktari wengi au wauguzi wengi wale wengine wanatoka huko huko Mnazimmoja au hospitali za Serikali huko wanakuwa laini kule kwetu katika Serikali wanakuwa wagumu, jee hapa pana nini namuomba Mhe. Waziri atafute kitu gani kinasababisha matokeo hayo yanayootokea. Mnazimmoja hana wakati lakini katika hospitali binafsi katulia ana kubembeleza kama mtoto umezaliwa leo. Kwa hivyo niseme Mheshimiwa kuna namna ya makusudi ambayo inasababisha kwamba baadhi ya watendaji wetu katika hospitali wanajali ubinafsi kuliko mengineyo.

Mheshimiwa hii nasema nikiumwa na mimi nakimbilia huko huko Mnazimmoja nisije onekana Shihata alisema mabaya sina nia hiyo nimesema baadhi na hakuna kitu kizuri kwa Mwenyezi Mungu kuliko kusema ukweli, baadhi sio wote.

Mhe. Mwenyekiti, hili nakuomba sana Mheshimiwa uliangalie na tulifanyie kazi *sector* binafsi wanafanya vizuri na wanahudumia watu vizuri na wanapata mahitaji yao vizuri kwa hivyo tuwapongeze kwa kazi zao nzuri, lakini pia

hospitali za vijijini na hawa pia tunawapongeza kwa kazi zao nzuri hatujapata malalamiko makubwa kama Mnazi mmoja.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, naombi kwa Mhe. Waziri kama lifuatalo Mhe. Shamsi Vuai Nahodha alipokuwa Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe lakini pia alikuwa na Mhe. Haji Juma Sereweji Mhe. Mbunge mstaafu wa Jimbo la Mwanakwerekwe wakati huo, walifanya kazi moja kubwa sana ili kuwaondolea wananchi wetu shida wakajenga Kituo cha Afya Magirisi Taveta. Kituo hicho Mheshimiwa mimi baada ya kwenda katika kampeni zangu nilikula ahadi kwa wananchi wangu nikasema mimi kwa hali na mali nitapigana kwa uwezo wangu wote Serikali na wahisani wowote lakini kituo kile kimalizwe ili akina mama wajawazito wajifungue pale, watoto wetu wapimwe pale, lakini pia na wazee wengine wapate matibabu pale karibu.

Na hili lilinipa nguvu Mheshimiwa baada kuona jirani zetu wa Fuoni hospitali ya Fuoni ina mzigo mkubwa sana ya wagonjwa namuhakikishia Mhe. Waziri hospitali nimeipiga plasta nje na ndani tayari imemalizika, madirisha na venti zote tayari, mlango wa mbele na wa nyuma tayari tumebakiwa na *ceiling board* na *tiles* chini, namuomba kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wananchi wameridhika sana na utendaji uliotokea na wanaipongeza Wizara ya Afya kama itawasaidia palipo bakia asilimia thamanini na nguvu za wananchi naweza kusema hivyo lakini iliyobakia ndogo sana Mheshimiwa *gypsum* tu juu *tiles* chini tufanye angalau wananchi wetu waridhike.

Lakini najua Mheshimiwa una nafasi nzuri, una wahisani wazuri nawapongeza wahisani wetu wote wa mashirika mbali mbali ya kimataifa na ya ndani waliokuwepo katika nchi yetu wanosaidia huduma za afya katika nchi yetu. Mheshimiwa hospitali hii italeta huduma nzuri kwa wananchi wetu na itasaidia mzigo mzuri kwa watu Fuoni kwa sababu madaktari wa Fuoni nawapongeza wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini wanafanya kazi usiku na mchana bila ya kuchoka.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nitalolizungumza hii hospitali ya Fuoni hawa ni majirani zetu wanafanya kazi nzuri nawapongeza wazuri hawana maudhi kwa wananchi wetu lakini wana shida moja tu Mheshimiwa naomba kurudia hapa kuisema, wanalalamikia juu ya gari ya wagonjwa ya kituo ambayo ilitolewa na Mwakilishi wa jimbo lile, Mbunge mstaafu wa Jimbo la Fuoni ndugu yetu Said Zuberi, lakini bahati mbaya gari ile huduma zake Mhe. Mwenyekiti inatumiwa madaktari wachanganyishane pesa za mafuta kwa hivyo naiomba Serikali kupitia Wizara hii iwaangalie na iwasaidie kwa hali na mali. Dereva hana malipo rasmi, mafuta hayapo rasmi waingize kwenye mradi wao

au kwenye Taasisi yao kama ni chombo cha Wizara ambacho kinafanya kazi kwa niaba ya wananchi wetu wakwenda kupata huduma pale hasa wazazi.

La mwisho Mheshimiwa baada ya hayo yote baada ya kuomba Mhe. Waziri kanisikia vizuri sana juu ya Hospitali ya Taveta Magirisi naomba kutoa kauli kwamba hivi sasa hivi kama tulivyoambiwa kwamba kuna mripuko wa maradhi ya kipindupindu, lakini hali ya mazingira yetu machafu kwa hivyo naiomba Wizara itowe zaidi wito au itowe kauli za kuhakikisha wananchi wetu wanakwenda na shughuli zao kuweka vyakula vyao safi, pazuri bila ya matatizo.

Lakini kwa kuwa Serikali imetangaza vyakula vya maji maji vyakula vizuiliwe sina pingamizi nalo lakini kwa wale walioruhusiwa vyakula vikavu watafute masanduku mazuri na waweke mazingira safi ili wandeleze shughuli zao kwa sababu tukizingatia kwamba riski zao wanategemea biashara zao.

Baada ya hayo Mheshimiwa kwa heshima kabisa naunga mkoni asilimia mia moja hotuba hii na yale yote niliomuomba Mhe. Waziri wa kuyafatilia wayafatilie ile adha iondoke na maombi ya kumaliziwa kituo changu kipya cha Magirisi Taveta kimalizwe ili wananchi wetu wapate faraja ya matumizi na matunda ya Wabunge waliopita na Wawakilishi pamoja na mimi Mwakilishi nilokuwepo naunga mkono hoja. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Shihata Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kijitoupele kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis Nafasi Maalum za Watu wenye Ulemavu kipitia Kusini Unguja na baadaye kama muda upo nitampa nafasi Mhe. Abdalla Diwani kama muda utaruhusu.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia machache bajeti ya Wizara hii ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizarza hii kwa jitihada zao wanazozichukua katika kuhakikisha afya za wananchi zinaimarika.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kutoa pongezi za pekee kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuimarisha sekta ya afya na sote ni mashahidi miongoni mwa sekta ambazo Mhe. Rais ameziimarisha kwa kiasi kikubwa ni sekta hii ya afya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa huduma zilizoimarishwa katika Wizara hii ni huduma ya mama na mtoto kwa kufunguliwa majengo mapya ya Unguja na Pemba, lakini vile vile kuhakikisha kwamba dawa au vile vitu muhimu vya kuimarisha huduma hii vinapatikana. Lakini vile vile katika kuboresha huduma hii nisiwe mkosefu wa fadhila kwa kuacha kuwapongeza wafanyakazi wetu wakiwemo wauguzi na madaktari kwa jitihada yao ambayo wanaifanya ili kuhakikisha kina mama wajawazito afya zao zinaimarika na wanajifungua salama. Pamoja na pongezi hizo katika utoaji wa huduma hii bado kuna changamoto.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ni utaratibu wa utoaji wa huduma hauko katika *formula* maalum. Mhe. Mwenyekiti, nitoe mfano kwa hivi sasa mama mjamzito anapokwenda kupima ujauzito katika hospitali zetu hizi basi mama yule hulazimika kulipa shilingi 7000/-. Mhe. Mwenyekiti, shilingi 7000/- hiyo anaambiwa sijui anapimwa wingi wa damu, sijui anapimwa sukari, anapimwa *pressure*, anapimwa mkojo. Lakini utizama mama yule ujauzito ule unapopea kwa wingi anakwenda mara moja, na kila wiki anayokwenda alipe shilingi 7000/-. Kwa hiyo, utaratibu bado haujakaa vizuri na hasa tukisema huduma za mama wajawazito zitatolewa bure wananchi wanaelewa hivyo.

Kwa hiyo, ikitokea vyenginevyo patahitajika ufafanuzi wa kutosha na kwa hili nimuombe Mhe. Waziri atapokuja kufanya majumuisho aje atueleze kwa faida ya sisi waheshimiwa tuliomo humu lakini vile vile kwa wale wananchi ambao wanatusikiliza hususan wanawake, na kina baba pia kwa sababu wao kina baba pengine ndio wanaoitoa hiyo shilingi 7000/-. Tukiangalia hali zetu za kimaisha wengine wanaimudu hiyo 7000/- lakini wengine hawaimudu, na kama haimudu kitachopelekea mama yule atashindwa kwenda hospitali kupata ile huduma ya kupima ujauzito wake. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nikuombe tu utakapokuja hapa uje utupe ufafanuzi wa kutosha juu ya hili kama hii ni halali au inafanywa tu kwa bahati mbaya na watendaji wachache au kama inafanyika, inafanyika hivi kwa sababu gani.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika huduma za mama wajawazito nije katika kile kitengo ambacho tunakwenda kule mama wajawazito siku ya mwisho ile ya kujifungua tunategemea ndio tunashusha ule mzigo. Mhe. Mwenyekiti, wanajitahidi sana watendaji wetu wauguzi na wakunga, lakini kuna changamoto nyingi pale. Tunalaumu hospitali ile ni chafu, tunasema hospitali mpya sasa hivi ni chafu na chafu kweli hairidhishi, lakini changamoto iliyokuwepo pale mimi mwenyewe nilikuwa shahidi nimekwenda pale watendaji nao ni kidogo wanaofanya ule usafi na jengo lile kubwa, wanawake

mle tunakwenda wengi. Mhe. Mwenyekiti, utakuta mtu anayefanya usafi ni mmoja yule ni binadamu anafika wakati anachoka. Lakini vile vile kwa wale wakunga wenyewe wanakuwa wapo kidogo, sisi kina mama tunajijua wenyewe harakati zetu wakati wa kujifungua, huku anaitwa, huku anaitwa, huyu huku anajifungua, huyu huku anajifungua mtu mmoja atafanye hao watu wawili?

Kwa hili nimuombe Mhe. Waziri akaangalia sana kitengo kile kuwaongezea wauguzi, tutakuwa tunalalamika huduma sio nzuri, huduma ni nzuri lakini watendaji ni kidogo, wanafika pahala hawajui wafanye nini sisi wenyewe ndio wanawake tunaoingia mle tunaiona ile hali wanajitahidi lakini linapotokea tatizo ndio hapo, kwa sababu mtu mmoja anatakiwa ahudumie wodi nzima ile pale, inakuwa tabu au watu wawili inakuwa ni tabu. Wakati mwengine watu watatu wanajifungua kwa wakati mmoja hali inakuwa tete, lazima Mhe. Waziri pale tuwafikirie kwa kuwaongezea wauguzi na vile vile wale wafanyakazi ambao wanafanya usafi ili ile lawama ya kuwa jengo chafu, hospitali chafu iondoke.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo katika jengo lile la kinamama ambalo wanakwenda kujifungua. Mhe. Mwenyekiti, jengo lile limejengwa juzi tu lina mwaka mmoja, lakini huko nyuma nakumbuka tulikuwa tukilalamika kwamba hakuna sehemu ya wale wanaopeleka wazazi wao sehemu ya kusubiria, kwa sababu wakati mwengine unampeleka mzazi unataka uwe karibu kusubiri. Kinachofanyika sasa hivi wale wanaopeleka wazazi wao wakesha wanaambiwa watoke nje wende kwenye jengo la Wizara ya Afya wakasubirie kule. Lakini tukiangalia mle ndani mna vibaraza vimejengwa kwa mtizamo wangu mimi nilivyoviona vile vibaraza nimehisi kwamba wasikae ndani kuwapa joto wale wagonjwa na wawaache wale wauguzi wafanye kazi zao watoke pale nje wasubirie kwenye yale mabenchi yaliyojengwa pale.

Lakini kinachofanyika akikalia lile benchi pale wanafukuzwa wote. Mhe. Mwenyekiti, tutizame mvua kama hizi mtu unamtoa pale mzazi wake yumo ndani unamwambia aende Wizara ya Afya kwenye muembe, karibu na Majestic kule akakae mvua kama hizi magonjwa ya mripuko mengi au anaambiwa akakae kule Maisara kwenye miti katika hali ya kawaida binadamu wa kawaida kweli ataweza kukaa katika mazingira kama yale, hali hairidhishi. Mhe. Waziri ningekuomba utakapokuja hapa kwa faida yetu sisi na wananchi ambao tunawawakilishi uje utwambie yale mabenchi yaliyojengwa katika jengo jipya mle ndani yamewekwa kwa madhumuni gani? Kwa ajili ya wale waliopeleka wagonjwa wao kusubiria pale au kwa ajili ya wauguzi au wafanyakazi wengine kuja kukaa pale. Naomba ufafanuzi wa hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika huduma za uzazi wa mpango. Mhe. Mwenyekiti, huduma hii ni nzuri na imetusaidia sana wanawake tumeweza kuimarisha afya zetu na kuweza kudhibiti uzazi. Kwa kipindi hiki chote si wanawake wengi ambao wanazaa hapo kwa hapo, na naamini yale ma-*nutrition* mengi yamepungua. Lakini Mhe. Mwenyekiti, huduma hii sasa hivi imekuwa inatolewa kwa mimi nahisi kinyume na utaratibu. Kwa sababu ninavyokumbuka mimi huduma hii unapotaka kupatiwa kuna uchunguzi unafanyiwa kama mama ili kupatiwa huduma hizi. Unaangaliwa uzito wako, unaangaliwa afya yako, unaulizwa magonjwa gani ulionayo ili ujuulikane njia gani upewe. Lakini sasa huduma hii ya uzazi wa mpango inatolewa katika maduka yetu ya madawa ya binafsi. Mhe. Mwenyekiti, wasiwasi wangu huduma hii itatumika kwa wale ambao pia hawahusiki, kwa sababu huduma hii inapotolewa katika hospitali za binafsi au maduka ya madawa ya binafsi mtu anakwenda tu na pesa yake, mtu yeyote mwenye miaka 15, mwenye miaka 16, mwenye maradhi, aliyekuwa hana maradhi na atapewa kwani hakuna uchunguzi wowote utakaofanyika. Kwa hivyo, watapewa wanaohusika na wasiohusika.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wasiwasi baadae yasije yakatokea madhara na ikaonekana kwamba huduma hii haifai kutokana na matumizi mabaya ambayo yatakuwa yanafanywa, na naamini hilo litafanyika, kwa sababu mtu atakwenda pale atanunua na atapewa na atakwenda kutumia. Lakini sasa hapati kuelimishwa wala hapati kufanyiwa uchunguzi yeye anakwenda akinunua akila. Matokeo yake yatakuja kutokea madhara ambayo yataweza kusababisha watu wazichukie hizi dawa na kumbe vile inakuwa ni utaratibu mbovu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kwa hili alizingatie na aweze kulichukulia hatua kama tumekusudia huduma za uzazi wa mpango tunatoa katika vituo vyetu, basi kwa maduka ya binafsi vizuiliwe kwa lengo la kunusuru afya za mama.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije katika kitengo cha *physiotherapy*. Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki kipo enzi na enzi tena kitengo hiki ni muhimu sana kwa wananchi wote, kwa sababu anayepata ajali, anayepata homa marekebisho yanafanyika pale, panafanywa marekebisho anafanyiwa mtu mazoezi ya viungo. Lakini kitengo hiki kwa sisi watu wenye ulemavu ni kitengo muhimu katika maisha yetu, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti ulemavu sio maradhi au sio ugonjwa. Ulemavu hautibiki, matibabu ya ulemavu ni marekebisho mtu akiwa mgonjwa atatibiwa kwa vidonge au atafanyiwa operesheni atapoa. Lakini akiwa mlemavu hata apewe vidonge vya dunia nzima hapoi ulemavu umemganda pale pale. Kwa hivyo, kitengo hiki kipo pale sisi kinatusaidia, mtu wingu likipinda mguu umekacha anakwenda pale anapata kupigwa moto ananyooshwa, mguu umepinda anafungwa *splint* pale. Mhe. Mwenyekiti, lakini

cha kusikitisha kitengo hiki zaidi ya miaka mitatu au minne sasa hivi kinapangiwa bajeti lakini hakipewa hata shilingi moja. Kibaya zaidi katika bajeti hii nimeangalia hakijazungumzwa kabisa sijaona. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri pengine nimepitia kwa wahka atakapokuja yeye anifafanulie kiko wapi na kimepangiwa bajeti ya kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo hiki kutokuzungumzwa katika bajeti hii kimenisikitisha sana kama mimi, kwa sababu anayevaa kiatu ndio anajua namna gani kimembana. Kitengo hiki sisi watu wenye ulemavu kinatusaidia sana, na ukitizama hali zetu sisi watu wenye ulemavu wengi hawana uwezo. Naamini serikali imeweka kitengo hiki kwa makusudi, leo kitengo kile hakina pesa, mtu mwenye ulemavu anataka kufungwa *splint* uwezo wa kununua vifaa hana anarudi hapati huduma. Sasa hivi maajali tele tunalazimika watu wasafiri waende Dar es Salaam wakatengenezewe miguu bandia wakati kitengo kile tunacho na tuna wataalamu wazuri sana pale, na hawako wengi ni wachache. Kwa nini tusikiimarishe kile kitengo chetu ili na sisi tukaweza kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi serikali yetu kupitia ilani ya Chama cha Mapinduzi imeeleza wazi zitaimarishwa huduma za watu wenye ulemavu. Mhe. Waziri inakuwaje leo kitengo kile sijakusikia kukizungumza ndani ya kitabu chako, wakati wizara zote zinaweka utaratibu wa kuimarisha huduma kwa watu wenye ulemavu. Mhe. Waziri itakuwa hatukuelewi, nitakuelewa tu pale ambapo utakuja kunipa ufafanuzi wa kutosha juu ya kitengo hiki, kwa sababu sisi watu wenye ulemavu ndio kimbilio letu hapa hatuna kwengine. Kukosekana huduma katika kitengo hiki sisi tunapata madhila makubwa sana, kwa sababu tunategemea ma-*NGO's* na wao wanategemea wafadhili ndipo wafanye kazi, wafadhili wenyewe ndio hivyo, tukikosa wafadhili wapi tutapata huduma ya marekebisho na kutengenezewa viungo bandia. Mhe. Waziri nikuombe sana uje unipe ufafanuzi wa kutosha juu ya kitengo hiki kwa nini hamukiingizii bajeti ili wakaweza kusaidia na wakatoa huduma kwa watu mbali mbali, lakini na kwa nini sikukusikia kukitaja kwenye kitabu pia uje unieleze.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika bima ya afya…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie muda umeisha, kama utakuwa bado dakika zimemalizika, naomba umalizie muda umekwisha.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na haya masikitiko ambayo nimeyaeleza nalizuia fungu hili la waziri mpaka atakaponipa maelezo ya kina na ya kuniridhisha. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis nafasi za watu wenye ulemavu kwa kuwakilisha vyema, lakini Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuakhirisha Baraza naomba niwakumbushe tunaendelea na kikao siku ya Jumamosi kesho kama kawaida. Lakini kuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii Mhe. Ali Suleiman Ali anawatangazia wajumbe wote leo kamati hiyo itakuwa na mkutano muda wa saa nane katika ukumbi mnaokutana, saa nane mchana.

Waheshimiwa Wajumbe, na mimi nawashukuru sana kwa utulivu wenu pamoja na michango yenu lakini shukurani za pekee zimuendelee Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na muwasilishaji wake, na pia nimshukuru kabisa Mhe. Waziri wa Afya kwenye hotuba yake na uwasilishaji wake. Waheshimiwa naakhirisha kikao mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 5:57 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 03/06/2017 saa 3:00 asubuhi)